SportPesa
TZS. 468,576,020
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Bil.** 63/- zakusanywa tozo miamala ya simu ndani ya miezi miwili

UKURASA 3


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Ni kilio, watoto bilioni 1 hatarini athari mabadiliko ya tabianchi
UVIKO-19 unavyoitesa sekta ya madini
Wanakijiji hawa wanapolizwa na mengi...
•Kukosa usingizi, kuchangia maji na mifugo, wanyama pori

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Septemba 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580691

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Mbowe agonga mwamba tena kesi ya ugaidi

UKURASA 2

UKURASA WA 3

## BODI YAONGEZA MUDA MAOMBI YA MIKOPO

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imeongeza muda wa uombaji wa mikopo hadi Septemba 15 mwaka huu.
Pia, imesema kwa waombaji wanaoendelea na mafunzo katika kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), watapata fursa ya kuomba mkopo kwa siku 10 kuanzia Septemba 20 hadi 30 mwaka huu...



UKURASA WA 4

## POLISI YAENDELEA KUSHIKILIA BAADHI NDUGU WA HAMZA

JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, limesema linawashilikia baadhi ya...

UKURASA WA 19

## MAKINDA AONYA SIASA KATIKA SENSA

SPIKA Mstaafu wa Bunge, Anne Makinda, ameonya wananchi kuingiza masuala ya kisiasa kwenye sensa ya watu na makazi, inayotarajia kufanyika mwakani na ile ya majaribio itakayofanyika mwezi huu.
Makinda ambaye ni Kamisaa wa Sensa Tanzania, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wakazi...



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akiwapungia mkono wafuasi wake wakati akiingia kwenye gari la Magereza kurejea mahabusu, baada ya kesi inayomkabili ya ugaidi kuahirishwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakazi 644 Magomeni Kota kuingia nyumba mpya Oktoba

UKURASA 3



# Chanjo ya mifugo yazua balaa

- **Ng'ombe**, mbuzi wafa, mimba zaharibika, Waziri ataka TAKUKURU ihusike...

*Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** SIMBA QUEENS KUIVAA FAD KAMA FAINALI MBIO TIKETI CAF UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kinondoni, Harold Maruma (kushoto), akiangalia mashine maalum ya kupozea joto takataka zilizohifadhiwa katika kiwanda cha kuchakata mbolea cha Mboji, Mabwepande, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, wakati Kamati ya Siasa ya Chama hicho ilipofanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali katika wilaya hiyo juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbowe agonga tena mwamba kesi ugaidi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imetupilia mbali pingamizi la mawakili wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu na kusema inayo mamlaka kamili ya kusikiliza kesi za ugaidi.

Mvutano mwingine umeibuka baada ya uamuzi huo, upande wa utetezi umepinga kusomwa kwa hati ya mashtaka kwa madai ina kasoro zisizorekebishika, hivyo wanataka mashtaka yaondolewe.

Uamuzi ulitolewa jana mbele ya Jaji Elinaza Luvanda, baada ya kupitia pingamizi la kwamba mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri la ugaidi kwa sababu ni mahususi kwa mashtaka ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Akitoa uamuzi alisema anakubaliana na kanuni ya jumla kwamba pale panapokinzana kati ya sheria ya jumla na sheria mahususi, basi sheria mahususi inapewa kipaumbele.

"Ni kweli sheria namba tatu ya ugaidi inatoa tafsiri ya Mahakama kuwa ni Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama Kuu Zanzibar, kifungu namba 21 na 22 cha sheria hiyo havikufanyiwa mabadiliko, pia makosa ya ugaidi yalichotwa na kuwa makosa ya Uhujumu Uchumi.

"Inanilazimu kufuata mkondo mwingine kwa mazingira yaliyomo katika shauri hili ili kuleta suluhisho," alisema jaji.

"Maoni yangu Bunge lilidhamiria mahakama hii kusikiliza mashauri yaliyomo chini ya sheria ya ugaidi na kwamba kifungu namba 21 na 21 kutofanyiwa mabadiliko haikuwa na nia ya kuiondolea mamlaka," alisema.

Alisema kwa kufanya marejeo kifungu namba 107 cha Sheria ya Ardhi kabla ya marekebisho, mamlaka ya kusikiliza mashauri ya ardhi ilipewa Mahakama Mahususi ya Ardhi na kuondolewa mamlaka mahakama zingine.

Jaji Luvanda alisema sheria ya kazi pia imetoa mamlaka kwa Mahakama ya Kazi.

"Kama ingekuwa sheria namba 21 ya mwaka 2002 au sheria namba 3 ya mwaka 2016 ingetoa mamlaka mahusus kwa Mahakama fulani kusikiliza mashauri chini ya sheria ya ugaidi hoja ya pingamizi ingekuwa na nguvu.

"Hizo sheria zinatoa mamlaka mahususi ya kusikiliza mashauri ya ugaidi hivyo hiyo hoja haina mashiko," alisema Jaji Luvanda.

Mahakama ilikubaliana na upande wa Jamhuri kwamba Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi inayo mamlaka ya kusikiliza mashauri ya ugaidi hivyo haikubaliani na pingamizi.

Upande wa Jamhuri unawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, Nassoro Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin na Wakili wa Serikali Tilimanyo Magige.

Upande wa utetezi unawakilishwa na Wakili Peter Kibatala, Jeremiah Mtobesya, John Mallya, Jebra Kambole, Frederick Kihwelo, Sisty Aloyce, Selemani Matauka, Nashon Mkungu, Michael Rugina, Bonifasia Makungu, Alex Maseba, Faraja Mangula, Michael Mwangasa na Gaston Shundu.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfan Bwire, Adam Kasekwa, maarufu Adamu na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

Katika shtaka la kwanza wanadaiwa wote, walikula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020, katila Hoteli ya Aishi iliyopo Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta kuhatarisha usalama wa taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Shtaka la pili wote wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi na kutaka kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Sabaya.

Shtaka la tatu, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali hapo aliwawezesha kifedha Halfani, Adamu na Ling'wenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi

kwa kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Shtaka la nne wanadaiwa kushiriki vikao vya kufanya vitendo vya kigaidi.

Shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5, mwaka 2020 eneo la Rau alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger.

Mshtakiwa Halfani katika shtaka la sita anadaiwa Agosti 10, mwaka 2020, kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi alitumia sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na Jeshi la kujenga Taifa(JKT) ambazo ni suruali moja ya JKT, pamoja na suruali nne za JWTZ, fulana moja, Koti la mvua moja, jacket moja, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

Baada ya uamuzi huo upande wa Jamhuri ulitaka kuwasomea washtakiwa mashtaka na maelezo ya awali, lakini upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Kibatala walipinga kwa madai kuwa hati ya mashtaka ni batili.

Kibatala alidai kitendo chochote kuhusiana na kosa la ugaidi kinatakiwa kuwekwa wazi ili kuweza kuunga mkono shtaka la ugaidi kwa mujibu wa maana ya sheria ya ugaidi, kushindwa kufanya hivyo kunafanya mashtaka kuwa na dosari za kisheria zisizoweza kurekebishika hivyo yaondolewe.

Wakili Jeremiah Mtobesya alidai mashtaka yamejirudia kwa kuwa mashtaka ya kula njama yako mawili na kuna shtaka lingine la kushiriki mkutano ambalo pia linajitegemea.

Alidai, kufanya mkutano ndio chanzo cha kosa la kula njama, lakini mashtaka hayo yamewekwa yakiwa yanajitegemea kitu ambacho ni kosa.

Upande huo wa utetezi unadai mahakama

inakosa mamlaka ya kuendesha mashtaka yanayowakabili washtakiwa kwa sababu masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Kuzuia Ugaidi namba 21 ya mwaka 2002 kinachoweka zuio dhidi ya makosa ya ugaidi Tanzania hakifafanui ni vitu gani vinatengeneza ugaidi.

Wakili Robert alipotakiwa kujibu aliomba Mahakama iwape muda upande wa Jamhuri kupitia hoja ili wajibu.

Mahakama ilikubali kuahirisha kesi hiyo hadi kesho kwa ajili ya upande wa Jamhuri kujibu hoja za utetezi za kupinga hati ya mashataka wakidai ina kasoro.

# Chanjo ya mifugo yazua balaa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameagiza kusakwa na kufikishwa kwenye Baraza la Veterinari Tanzania (VCT) wataalamu wa mifugo waliotoa chanjo katika Kijiji cha Mlazo wilayani Chamwino na kusababisha baadhi ya mifugo kufa na mingine kupata madhara.

Pia ameagiza kampuni ya Agristeps Limited iliyoingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa ajili ya kusimamia utoaji chanjo, kuzuiwa kuendelea na kazi hiyo na kufikishwa kwenye baraza hilo kwa uchunguzi zaidi.

Waziri Ndaki alitoa maagizo hayo juzi alipofika katika kijiji hicho baada ya kupata taarifa juu ya madhara yaliyojitokeza baada ya mifugo hiyo kupatiwa chanjo.

Alisema mifugo hiyo ilichanjwa homa ya mapafu (CBPP) na ng'ombe 25 wamekufa, 33 mimba ziliharibika na waliovimba sehemu waliyochomwa sindano 58. Pia mbuzi mmoja amekufa, waliovimba watano, waliotoa mimba 12 huku kondoo waliokufa 20, waliovimba 16 na waliotoa mimba watano.

Waziri huyo alisema licha ya utoaji chanjo hiyo kuendelea vizuri nchini, amesikitishwa katika kijiji hicho haikufanywa kwa kuzingatia kanuni za kitaalamu.

"Wale wataalamu waliochanja ng'ombe wa hawa watafutwe majina yao, wamesomea wapi, wapelekwe kwa Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania. Hatuwezi kuendelea kuua ng'ombe namna hii. Hii kampuni ilitakiwa ijiridhishe na utaratibu na mchakato mzima wa uchomaji wa chanjo kwa kuwa amefanya kazi hii hapa kuwa mbovu asimame kuendelea kutoa chanjo kwenye wilaya ya Chamwino, tafuteni mwingine," alisema.

Pia alizitaka halmashauri zote nchini kuhakikisha watoa huduma walioingia nao mikataba ya utoaji chanjo za mifugo dhidi ya magonjwa 13 ya kimkakati, yanafuata taratibu na kuzingatia miongozo ya wizara.

"Kuna haja ya kubadilisha Sheria ya Veterinari ya Mwaka 2003 na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama ya Mwaka 2003 ili endapo mifugo ikipata madhara yoyote mfugaji aweze kufidiwa mifugo," alisema.

Aliutaka uongozi wa Wilaya ya Chamwino kutoendelea kutoa chanjo katika kijiji cha Mlazo hadi wataalamu watakapotoa elimu ya kutosha kwa wafugaji hao kwa kuwa kwa sasa wamekosa imani.

Waziri aliwaonya watu wanaotumia kigezo cha wafugaji kuwa chanzo cha mapato yao binafsi kwa kuwalipisha faini zisizo halali na kuagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Chamwino kusimamia suala hilo kabla hajalipeleka katika ngazi ya juu zaidi.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, alisema uchunguzi uliofanywa umebaini kuwa sindano zilizotumika zilikuwa ndefu na kwamba mifugo ilipaswa kuchomwa chini ya ngozi maeneo ya shingoni ambapo kuna ngozi nene na si kwenye mguu.

Prof. Nonga alisema chanjo imeelekeza kuwa endapo ikiingia ndani ya nyama inasababisha nyama kuharibika kwa kuwa inaua seli za mwili kama ambavyo imefanyika kwa baadhi ya mifugo kupata uvimbe, majipu na usaha maeneo ambayo imechomwa chanjo.

# Neema yaja wakazi 644 Magomeni Kota

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI wa Magomeni Kota mkoani Dar es Salaam, wamepata matumaini mapya, baada ya kuahidiwa kuhamia makazi mapya Oktoba mwaka huu.

Habari hiyo njema kwao imetokana na kikao kati ya viongozi wao na wa serikali.

Juzi Nipashe ilipata taarifa kwamba viongozi wa serikali walikutana na viongozi wa wakazi hao kujadili kuhusu hatima ya suala hilo, baada ya mwishoni mwa wiki kufikisha kilio hicho kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia vyombo vya habari.

Mwenyekiti wa wakazi wa Magomeni Kota, George Abel, akizungumza na Nipashe jana, alisema, katika kikao cha juzi kati yao na serikali walikubaliana wahamie kwenye makazi mapya mwezi ujao, huku ujenzi ukiendelea kukamilishwa kwenye maeneo madogo.

"Mwezi wa 10 tutahamia, sasa hivi wanakamilisha ufungaji wa transifoma na mita za Luku kwenye kila 'appartment. Serikali imesema tupuuze kauli juu ya udhalilishaji na imesema inatambua wakazi 644 na sio 300 kama ilivyoelezwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari," alisema Abel.

Mwishoni mwa wiki, Nipashe iliripoti taarifa kuhusu wakazi hao, wakimwomba Rais Samia kutoa neno kuhusu makazi hayo, wakidai ujenzi umekamilika na siku za wao kuhamia zikizidi kusogezwa mbele kila uchao, na kwamba baadhi yao wanaishi kwa ndugu, jamaa na wengine wakipanga.

Aidha, kwenye mkutano wa Jumapili, Abel alisema taarifa za hivi karibuni zilizoripotiwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari ni kati ya sababu mojawapo ya kuitisha mkutano huo.

Abel, alidai taarifa hizo zilieleza kwamba wakazi ambao watahamia kwenye kota hizo ni 300 pekee badala ya 644 ambao ndio walisajiliwa kabla ya ujenzi kuanza na kuhakikiwa Februari, mwaka huu.

"Hivi karibuni tulishangaa kusikia taarifa za aliyekabidhiwa ujenzi kusema wanaotakiwa kuhamia ni 300 tu, wakati sisi tupo 644, tulihakikiwa Februari 15 mwaka huu, na barua kama kamati kwenda kwa Rais na Waziri Mkuu alikuja.

"Tunaomba Rais asikie kilio chetu, tuliambiwa tutahamia Agosti, lakini bado wanasema hadi Oktoba mwaka huu, ila kwa yanayoendelea tumeona tuyaseme," alisema Abel.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo kwa takribani miaka 25, Salama Goronga, alisema kama mmoja wa zilizokuwa Kota za Magomeni, wanamwomba rais atoe neno kuhusu makazi hayo mapya ambayo bado wanasubiri siku ipangwe ya kuhamia.

"Hayati Magufuli alisema tuliokuwa wakazi tutakaa miaka mitano bila kulipa kodi, baadaye kuzinunua kwa bei nafuu, Kwa sisi wakazi ambao tuliishi hapa na tukapisha ujenzi, leo hii waruhusiwe 300 pekee na sisi tuko zaidi ya 600 sio haki," alisema Salama.

Hata hivyo, Jumatatu, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliiambia Nipashe kwamba suala hilo linasubiri uhakiki wa majina ya waliokuwa wakazi halali kwenye kota hizo, hivyo wakazi hao wawe na subira.

## Bodi yaongeza muda maombi ya mikopo

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imeongeza muda wa uombaji wa mikopo hadi Septemba 15 mwaka huu.

Pia, imesema kwa waombaji wanaoendelea na mafunzo katika kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), watapata fursa ya kuomba mkopo kwa siku 10 kuanzia Septemba 20 hadi 30 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema wamefikia uamuzi huo ili kutoa fursa kwa waombaji ambao wamejisajili katika mfumo kukamilisha maombi yao.

Pia, alisema wamepokea maombi kutoka kwa makundi mbalimbali wakiomba waongezewe muda wa kukamilisha maombi yao.

Alisema hadi kufikia Agosti 31 ambayo ilikuwa siku ya mwisho wa kupokea maombi hayo, waliowasilisha maombi walikuwa 91,445 na kati ya hayo, maombi 12,252 yalikuwa hayajakamilika.

"Tulianza kupokea maombi kwa njia ya mtandao Julai 9, mwaka huu na hadi jana (juzi) ambayo ilikuwa siku ya mwisho ya kuomba tulikua na waombaji 91,445 waliowasilisha maombi, na kati ya hayo, maombi 12,252 yalikuwa hayajakamilika na wateja wetu wameomba muda wa kukamilisha," alisema Badru.

Badru alisema hatua inayofuata kwa sasa ni uhakiki wa nyaraka na taarifa zilizowasilisha na waombaji 79,193 ambao maombi yao yamekamilika.

"Kuna makundi mawili, wale 12,252 ambao maombi hayana viambatisho, hivyo hayajakamilika, na kuna maombi 79,193 yenye nyaraka, sasa tunaanza kuhakiki usahihi wake na baadaye tutaangalia kama wamepata udahili, na wale wenye sifa ndiyo watapangiwa mkopo," alisema Badru.

Kwa mujibu wa HESLB, katika mwaka wa masomo 2021/2022, serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 570 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi 160,000 wa taasisi za elimu ya juu na kati ya hao, wanafunzi 62,000 wanatarajiwa kuwa ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 98,000 wanaoendelea na masomo na kwamba bajeti kwa mwaka 2020/2021 ilikua Sh. bilioni 464 na zimewanufaisha wanafunzi 149,398.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mapato na matumizi ya fedha za makato ya miamala. Kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Khatibu Kazungu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Miamala yaingiza bil. 63/- serikalini kwa miezi miwili

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

SERIKALI imepata Sh. bilioni 63 kutokana na tozo zinatokatwa kwenye miamala simu ndani ya miezi miwili.

Julai 15, mwaka huu, serikali ilianza kutoza tozo hiyo ambapo hadi kufikia Jumanne, kiasi hicho kimekusanywa.

Pia kuanzia Septemba mosi, mwaka huu makusanyo yote ya asilimia 30 ya makato mapya miamala hiyo ya simu yataelekezwa kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na ununuzi wa madawati na viti vya shule.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ndiye aliyebainisha hayo jana kwenye mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dodoma.

Dk. Nchemba alisema serikali imefanikiwa kuvuna kiasi cha fedha kutokana na makato ya matumizi ya miamala ya simu tangu kuanza Julai mwaka huu.

Alibainisha fedha hizo za makato hayo zilielekezwa kujenga vituo vya afya kwenye tarafa zote ambapo kuna vituo vya afya 220 vinatarajiwa kujengwa maeneo hayo kwa ajili ya kusogeza huduma karibu na wananchi.

Alisema vituo vitakavyojengwa vitakuwa na uwezo wa kutoa huduma ya matibabu ya kawaida na huduma ya upasuaji.

Kadhalika, alisema fedha hizo za makato serikali ilielekeza kupelekwa kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa miundombinu ya barabara kwenye maeneo hayo .

Pia aliongeza kuwa makato hayo yataelekezwa kwenye kutatua tatizo la maji maeneo mbalimbali nchini ili wananchi waone manufaa ya kulipa kodi hizo kwa sababu faida yake itawarudia wenyewe.

Dk. Mwigulu alisema makato mapya ya miamala ya asilimia 30 yatakayoanza kukatwa kuanzia jana, yataelekezwa kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa

Alisema lengo la ujenzi huo ni kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kwenye shule za msingi kila mwaka na wanaochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari.

Dk. Nchemba alisema kutokana na tathmini iliyofanywa na serikali kuhusu ongezeko hilo, wameona waanze kupeleka fedha hizo huko ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa michango.

Aidha, alitoa muda wa miezi mitatu kwa halmashauri zote kuhahakikisha zinawalipa watoa huduma wanaodai kutoka miaka ya nyuma.

Alisema wapo watoa huduma ambao wameathirika kutokana na kuchukuliwa vitu vyao na benki zinazowadai, hivyo ilisababisha hata halmashauri kubadilisha watoa huduma, kutokana na kuogopa madeni kuwa makubwa kwa mtoa huduma mmoja.

# RC asema wanaoshindwa kutoa uamuzi wana matatizo ya lishe

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, amesema viongozi wanaoshindwa kutoa uamuzi sahihi na kwa wakati katika ngazi mbalimbali, wana matatizo ya lishe.

Aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha kujadili miradi ya ujenzi wa vituo vya afya na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali mkoani Mwanza huku akibainisha kuwa lishe duni inamfanya mtu ashindwe kutoa uamuzi sahihi na kwa wakati.

Mkuu huyo wa mkoa alisema suala la lishe halihitaji fedha nyingi kama inavyodhaniwa badala yake kinachotakiwa ni watu kupatiwa elimu kujua mpangilio wa vyakula vinavyotakiwa kwa ajili ya kupata lishe bora.

Aliagiza suala la lishe lipewe kipaumbele cha kwanza katika mkoa wake ili kuwasaidia wananchi kupata mlo sahihi ambao utajenga afya zao.

Gabriel alisema lishe bora inasaidia mtu kufikiri na kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati na kuwaagiza wataalamu wa afya kusaidia jambo hilo katika jamii mkoani Mwanza.

"Lishe ni kitu muhimu sana na wala hakihitaji fedha nyingi, kinachotakiwa na kutoa elimu kwa wananchi ili kujua namna ya kupangilio milo yao," alisema.

Pia mkuu huyo wa mkoa alishuhudia utiaji saini mkataba wa utekelezaji wa matumizi ya lishe kwa wananchi ili kujenga taifa lenye afya, kujijenga kiuchumi na kuepukana na magonjwa mbalimbali.

Alisema wamesaini mkataba kwa ajili ya lishe, hivyo isiwapo halmashauri ambayo haitotoa mchango wake kupitia bajeti zake.

"Usikute nao wanaotekeleza huu mpango ndani ya jiji wana changamoto ya lishe kwa sababu vionja vya tatizo la ukosefu wa lishe ni kushindwa kufikiri na kufanya maamuzi kwa sababu lishe bora inazuia kufanya maamuzi tukiwa na watendaji wengi wanaoshindwa kuelewa vitu kwa uharaka shida hapo ni lishe," alisema.

Wakati huo huo, Gabriel aliwaagiza wakaguzi ndani wa halmashauri kuangalia viashiria hatarishi katika miradi ambayo serikali imetoa fedha ili kunusuru upotevu wa mapato.

Alisema alizunguka halmashauri zote na kubaini wakaguzi walikuwa na tatizo la kutokagua miradi yote ambayo inatekelezwa ikiwamo ya serikali kuu.

Aliwagiza wakurugenzi kuhakikisha hawatumii fedha ambazo wamejihakikishia usalama wake bila kufanya hivyo ni hatari.

**•Imeandikwa na Richard Makore na Neema Emmanuel**



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akikata utepe kuzindua Kiwanda cha kuoka mikate cha Magereza, eneo la Msalato jijini Dodoma jana. Kulia kwake ni Naibu Waziri wa wizara hiyo, Khamis Chilo na (kushoto kwake) ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Suleiman Mzee. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# IPP Media yaongoza uteuzi tuzo EJAT

**Na Elizabeth Zaya**

WAANDISHI wa habari wa IPP wameongoza katika uteuzi wa tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2020 ambazo huratibiwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Kati ya wateule 59 waliotangazwa jana, waandishi wa IPP waliteuliwa ni 12 kutoka katika magazeti ya Nipashe na The Guardian.

Kwa mujibu wa orodha ya wateule iliyotangazwa jana Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Kajubi Mukajanga, kati ya waandishi 20 wanaoandikia magazeti walioteuliwa kuingia katika tuzo hizo, 12 ni kutoka katika magazeti ya Nipashe.

Walioteuliwa kutoka IPP ni Sanula Athanas, Renath Msungu, Elizabeth Zaya, Henry Mwangonde, David Chikoko, Christina Mwakangale na Jumanne Juma. Wengine ni Augusta Njoji, Jenifer Gilla, Mary Geofrey, Zuwena Shame na Muhidin Msamba.

"Safari hii jumla ya waandishi 59 wameteuliwa kati ya waandishi 147 waliowasilisha kazi zao.

Kati ya hao 20 wanaandikia magazeti, saba ni mitandao ya kijamii, na 33 ni kutoka radio na runinga. Yaani 20 radio na 13 TV, mmoja kati yao ameteuliwa toka magazeti na mitandao," alisema Mukajanga.

Na kati ya wateule hao, alisema 26 ni wanawake 10 wanatoka kwenye magazeti, wawili kutoka mitandao ya kijamii na 14 vyombo vya kielektroniki. Wateule wanaume ni 33 ambao 10 ni kutoka magazetini, 19 redio na runinga na watano ni mitandao ya kijamii.

Mukajanga alisema washindi wa tuzo hizo watajulikana rasmi Septemba 10, wakati wa kilele cha tuzo hizo kitakachofanyika jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Mukajanga, kilele cha sherehe za tuzo hizo mwaka huu zinatarajiwa kufanyika kwa njia ya mtandao kutokana na tahadhari ugonjwa wa UVIKO-19 na watakaoshinda watafuata zawadi zao katika ofisi za MCT kwa waliopo Dar es Salaam na kwa walioko mikoani watatumiwa.

Alisema wateule katika tuzo hizo walitokana na kazi 395 kutoka kwa waandishi wa habari nchi nzima zilizopokelewa kwa ajili ya kushindanishwa katika makundi 19 ya tuzo hizo.

Kati ya kazi hizo, 59 ziliwasilishwa na waandishi wa habari kutoka Dar es Salaam, 27 kutoka Kisiwa cha Pemba, Unguja 24, Mwanza 22, Dodoma 21 zikitoka katika vyombo 72 vya habari vikiwamo vikubwa na vidogo kama redio za kijamii.

Miongoni kwa makundi yanayoshindanishwa katika tuzo hizo ni tuzo ya uandishi wa habari za uchumi, biashara na fedha, habari za michezo na utamaduni, kilimo na biashara ya kilimo, habari za elimu, utalii na uhifadhi, habari za uchunguzi, takwimu, haki za binadanu na utawala bora.

Vipengele vingine vinavyoshindaniwa ni mpigapicha bora magazeti, mpigapicha bora runinga, katuni bora, afya, jinsia na watoto, walemavu, gesi, mafuta na uchimbaji madini, ubunifu na maendeleo, usalama barabarani, hedhi salama na kundi la wazi.

# Polisi yaendelea kushikilia baadhi ya ndugu wa Hamza

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, limesema linawashilikia baadhi ya watu kuendelea na uchunguzi dhidi ya tukio la Hamza Hassan.

Jumatano iliyopita katika eneo la Selander, Hamza ambaye sasa ni marehemu, aliwashambulia askari kwa kuwaua wanne na kujeruhi wengine sita na yeye kuuawa.

Kamanda wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, alipoulizwa na gazeti la Nipashe kuhusiana na uchunguzi dhidi ya ndugu wa Hamza ambao baadhi yao bado wanashikiliwa, alisema upelelezi unaendelea.

Kuhusu idadi ya wanaoendelea kushikiliwa hadi siku hiyo, kamanda Muliro alisisitiza kuwa, "upelelezi bado unaendelea."

Kuhusu majeruhi wa tukio hilo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Aminiel Aligaesha, alisema wote waliruhusiwa Jumatatu ya wiki hii.

Hamza kabla ya kuuawa aliwashambulia askari wawili waliokuwa kwenye kibanda maeneo hayo ya Selander kisha akachukua silaha zao mbili aina ya pistol na kuanza kurusha risasi ovyo na kusababisha vifo vingine viwili vya askari na kuwajeruhi watu sita.

Mauaji hayo yalitokea wakati Hamza akirushiana risasi na polisi karibu na Ubalozi wa Ufaransa hadi kupigwa risasi na kufa na polisi kushikilia baadhi ya ndugu zake akiwamo mama na wadogo zake kwa mahojiano, baadhi yao kuachiwa na wengine kuendelea kubaki.

Waliouawa katika tukio hilo ni askari watatu wa Jeshi la Polisi na mmoja kutoka kampuni ya ulinzi binafsi.

**Kamanda wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, alipoulizwa na gazeti la Nipashe kuhusiana na uchunguzi dhidi ya ndugu wa Hamza ambao baadhi yao bado wanashikiliwa, alisema upelelezi unaendelea.**

## TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.


| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mogas Kurasini Depot, S.L.P. 70284, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 310/03, Eneo la Kurasini, Manispaa ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam. | Michael Nduhuukire (Raia wa Uganda) | Leseni ya jumla ya mafuta |
| 2. | Tupesh Energy (T) Limited, S.L.P. 1254, Dar es Salaam. | Kiwanja Na 7, Kitalu "E" Eneo la Shekilango, Manispaa ya Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam. | Said Shaban Kondo (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta |
| 3. | Jambo Food Products Ltd, S.L.P. 71, Shinyanga. | Mtaa Ibadakuli industrial area, Kata ya Ibadakuli Wilaya ya Shinyanga Mjini, Mkoa wa Shinyanga. | Salum Khamis Salum (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 4. | Petroafrica (T) Ltd – Ngaramtoni Service Station, S.L.P 4878, Arusha. | Kiwanja Na. 3, Kitalu "A", Eneo la Oloirien, Kata ya Oloirien, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Mkoa wa Arusha. | Yasin Hersi Warsame (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 5. | SILYA OIL, S.L.P. 1056, Kahama. | Kiwanja Na. 942, Kitalu "B", eneo la Ibisabageni – Sengerema Mjini, Wilaya ya Sengerema, Mkoa wa Mwanza. | Masuke Shimba Kishiwa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Rulenge Filling Station, S.L.P. 03, Biharamulo. | Kiwanja Na.10, Kitalu 'B', Kijiji cha Chebitoke, Kata ya Kabindi, Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera. | Erasto Naakule (Mtanzania | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Lake Oil Kisukulu-Dar es Salaam, S.L.P. 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 179, Kitalu 'D', Eneo la Kisukulu, Manispaa ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 8. | Kwekuyu Energy Tanzania Limited-Mvuha, S.L.P. 45370, Dar es Salaam. | Eneo la Kota, Kijiji cha Dalla, Wilaya ya Morogoro, Mkoa wa Morogoro. | Alhaji Salimu Mdoe (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | Africa Energy (T) Limited-Vijibweni Petrol Station, S.L.P. 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 33, Eneo la Vijibweni, Manispaa ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Edha A. Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | Front Oil Filling Station, S.L.P. 360, Mwanza. | Kiwanja Na. 291, Kitalu "B", eneo la Buhongwa, Jijini Mwanza. | Fredy Simoni Upiro (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | Kiz Four Company Ltd, S.L.P 2196, Arusha. | Kiwanja Na. 20, Kitalu "B", Eneo la Nanenane, Kata ya Lemara, Halmashauri ya Jiji la Arusha, Mkoa wa Arusha. | Mercy Deogratius Makoye (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 12. | Aphi Distributors and General Traders, S.L.P. 1127, Bukoba. | Mtaa wa Zamzam, Kata ya Bilele, Wilaya ya Bukoba Mjini, Mkoa wa Kagera. | Audax Eustace Kaijage (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 13. | Salmo Oil Ltd, S.L.P. 732, Kigoma. | Kiwanja Na. 1163, Kitalu "A", Mtaa wa Kahabwa, Kata ya Kibirizi, Wilaya ya Kigoma - Ujiji, Mkoa wa Kigoma. | Mohammed Nassor Ally (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya LPG |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

216436001

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Uhamasishaji viwanda vipya uwe kipaumbele

**SOKO** la miti ya mikaratusi limeanza kuonekana katika baadhi ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, baada ya kuwapo kwa viwanda vya kuchakata miti hiyo, hatua ambayo inaweza kuchangia katika uchumi.

Miongoni mwa manufaa yatokanayo na hatua hiyo ni kusaidia kuinua kupato cha wakulima wa miti hiyo na serikali kupata kodi. Kuwapo kwa viwanda hivyo pia kunaweza kusaidia kuzalisha ajira kuanzia shambani hadi kwenye viwanda vya kuchakata miti hiyo sehemu mbalimbali nchini, hivyo kuinua uchumi wa Watanzania na taifa kwa ujumla.

Juzi, baadhi ya wakulima wa miti katika mikoa ya Iringa na Njombe, kwa nyakati tofauti waliliambia gazeti hili kuwa walianza kukata tamaa na kufikiria kuteketeza mashamba yao ya mikaratusi, kutokana na kukosa soko.

Hata hivyo, wanasema wamesitisha mpango huo, baada ya kuanzishwa kwa viwanda vya uchakataji wa nguzo za umeme kikiwamo kiwanda cha Qwihaya General Enterprises kwenye maeneo yao.

Kwa mujibu wakulima hao, kwa muda mrefu miti hiyo ilikuwa ikilimwa kwa matumizi ya kawaida kama kuni na mirunda kwa ajili ya ujenzi, lakini kwa kuwa thamani yake imeanza kuwa kubwa, baada ya kuwapo kwa viwanda vya kuchakata nguzo za umeme katika maeneo yao, wataendelea kuilima.

Kuwapo kwa kiwanda hicho cha kuchakata miti ya mikaratusi kwa ajili ya nguzo za umeme, tunashauri kwamba iwe ni fursa kwa serikali kuanza kuelekeza nguvu katika kuhamasisha uanzishaji wa viwanda mbalimbali kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Tunashauri hilo, kwa sababu si viwanda vya kichakata mbao tu vinahitajika, bali hata vya kuchakata mazao mbalimbali na matunda ambayo yamekuwa yakiozea mashambani kutokana na ukosefu wa soko.

Tunatambua lengo la serikali ni kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda ifikapo mwaka 2025, ndiyo maana tunashauri uhamasishaji wa kuanzishwa kwa viwanda zaidi hata vidogo vidogo kwa ajili ya kuchakata mbao na hata mazao mbalimbali.

Viwanda vikiwa vingi, tunaamini hata wakulima watalima mazao kwa wingi, kwani watakuwa na uhakika wa sehemu ya kuuza au kuchakata mazao yao na hawatakata tamaa kama ambavyo wale wa mikaratusi walivyotaka kufanya.

Kwa kuwapo uhamasishaji wa kuanzishwa viwanda vingi nchini, tunatarajia kuwa lengo la serikali la kuwa na Tanzania ya viwanda linaweza kuwa matokeo chanya, kwa sababu kwa namna moja au nyingine, kila upande utanufaika.

Viwanda vikianzishwa, vitalipa kodi, wakulipa watalima na wakiuza mazao nao watalipa kodi, viwanda vitakuwa na wafanyakazi, kwa maana kwamba watapata ajira kisha kuchangia katika maendeleo ya taifa kwa kulipa kodi.

Kulingana na mtiririko huo, ni wazi kwamba, nchi itaendelea kupiga hatua zaidi katika maendeleo kutokana na kodi itakayokusanywa kutoka katika vyao mbalimbali vikiwamo hivyo ambavyo tumevitaja.

Wito wetu kwa serikali ni kwamba ichukulie viwanda vya kuchata miti ya mikaratusi kuwa kichocheo cha kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vingi vya aina hiyo na vya mazao mengine zaidi.

Inawezekana kilimo cha miti hiyo hakiko mikoa ya Njombe na Iringa tu bali na mikoa mingine, ila kikwazo kinaweza kuwa ni sehemu ya kuiuza, ndiyo maana tunashauri kuwapo kwa viwanda vingi zaidi.

Wawekezaji katika viwanda wanaweza kuwa wa ndani au kutoka nje ya nchi, ili mradi Watanzania wafanye shughuli za kilimo wakiwa na uhakika wa sehemu ya kupeleka mazao yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Inahitajika elimu zaidi kukabili U.T.I kwenye jamii

**ELIMU** kuhusu maradhi mbalimbali hasa ambayo huwakumba zaidi wanawake, kutowafikia ipasavyo, ni kati ya sababu zinazosababisha kutoyatambua mapema na kuyatibu.

Hata hivyo, jamii bado imefungwa na wingu la dhana potofu kuhusu maradhi mengi yanayowashambulia wanawake na watoto.

Huku wataalamu wa afya wakisisitiza ni muhimu kufahamu dalili za maradhi husan maambukizi ya njia ya mkojo (U.T.I), ambayo hivi sasa huumiza wengi, bado watu wanashindwa kutofautisha ugonjwa huo na mengine.

Bingwa wa Magonjwa ya Kinamama na Uzazi kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Matilda Ngarina, anasema U.T.I kwa wanawake haimaanishi ni maambukizo ya sehemu za uke.

"Ukiwa kliniki kinamama wengi wanakwambia Dokta, U.T.I yangu ni sugu inajirudiarudia' . Jamii, au kinamama hawajui nini maana ya U.T.I, ukiongea naye mgonjwa huyu, anakueleza kuwa ni ute unatoka ukeni."

Anasema maambukizo ya njia ya mkojo au U.T.I hayatokei ukeni haya huanzia kwenye figo, hadi kwenye kibofu na sehemu ya kutokea mkojo. Wengi huchanganya maradhi ya ngono na ute unaotoka ukeni, ambao ni wa kawaida kwa mwanamke.

Anasema walio wengi hasusan wanawake huugua maradhi tofauti na kuyafananisha na maambukizo ya njia ya mkojo ambayo hata dalili zake haziendani. Kwa kinamama kuna ute unaotoka, ambao ni hali ya kawaida kwa kuwa ni mfumo wa kimaumbile.

Dokta Ngarina anasema wanaofika kliniki ya kinamama, hupewa elimu na kuelimishwa kuhusu tofauti ya maradhi yanayosababishwa na maambukizi kwenye njia ya mkojo na magonjwa ya ngono.

"Wanawake hudhani huambukizwa ugonjwa huu na wapenzi, waume zao, maambukizi njia ya mkojo hakuna uhusiano na hilo, kwa sababu wadudu hupita kwenye njia ya mkojo na si ukeni," anabainisha bingwa huyo.

Anaeleza kuwa ambao maradhi hayo hujirudia mara kwa mara huhitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi, ushauri na namna ya kuzingatia tibaa inayowafaa.

Kwa mujibu wa madaktari bingwa wa magonjwa ya uzazi pamoja na maambukizo ya njia ya mkojo husababishwa na vimelea au bakteria hatari, ambao huzidi uwezo wa kinga ya mwili katika mfumo wa mkojo. Maambukizi hayo yanaweza kuathiri figo, kibofu cha mkojo na mirija inayopita katikakati ya viungo hivyo.

Utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa U.T.I ni mojawapo ya aina za maambikizo yanayowakumba watu wengi zaidi duniani, takriban milioni 8.1 hufika hospitali au kliniki kila mwaka kuwaona madaktari kutokana na maradhi hayo.

Maambukizi ya mkojo yanaweza kugawanywa katika aina mbili ya njia ya juu na ya chini ya njia ya mkojo.

Njia ya juu inajumuisha figo na mrija unaopeleka mkojo katika kibofu (ureter) na njia ya chini ni ile yenye kibofu na mrija unaoelekea sehemu ya nyonga. Kwa wengi maambukizo ya njia ya mkojo husababishwa na bacteria, ambao kwa kawaida hupatikana katika mfumo wa mmeng'enyo wa chakula.

Kwa mujibu wa taarifa za mtandaoni, dalili za ugonjwa huu ni kadhaa ikiwamo kwenda haja ndogo kila mara, homa, kuhisi baridi, maumivu ya mgongo, mkojo mzito wenye harufu kali na mbaya zaidi na hata kukojoa damu

Wanawake wajawazito wanakabiliwa na uwezekano mkubwa wa kupata maambukizo kuliko wanawake wengine na yanapotokea yana uwezekano mkubwa wa kusambaa hadi katika figo, kwasababu mabadiliko mwilini wakati wa ujauzito yanaathiri njia ya mkojo.

Maambukizo miongoni mwa wanawake wajawazito yanaweza kusababisha hatari ya afya za wajawazito na watoto na hivyo, wanapaswa kufanyiwa vipimo kubaini uwapo wa bakteria katika mkojo wao, hata kama hawana dalili na kutibiwa.

Yote haya yanaonyesha kuwa inahitajika elimu kuhusu UTI na kuelimisha umma kuufahamu na kuukabili. Ikumbukwe kukinga ni bora kuliko kutibu.

HABARI PICHA

# MKURUGENZI MTENDAJI WA DSE MOREMI MARWA ATEMBELEA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kulia), akimkaribisha Mkurugenzi Mtendaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Moremi Marwa (wapili kushoto), baada ya kuwasili kwenye ofisi za kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**



Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Walles Maugo (kulia), akifafanua jambo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa DSE, Moremi Marwa (wapili kulia), alipotembelea chumba cha habari cha TGL.



Meneja wa kiwanda cha uchapishaji cha TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam, akitoa maelezo ya jinsi magazeti yanavyochapishwa kiwandani hapo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa DSE, Moremi Marwa.



Meneja wa East Africa Radio, Lydia Igavabuza, akitoa maelezo kwa wageni kutoka soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa (DSE), Moremi Marwa, kwenye ziara walipotembelea ofisi za East Africa Radio Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana.



Mhariri wa Habari wa ITV, Steven Chuwa, akifafanua jambo kwa wageni.



Mkurugenzi Mtendaji wa ITV na Radio One, Joyce Mhavile (kushoto), akitoa maelezo kwa wageni kutoka DSE, wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa DSE, Moremi Marwa, walipotembelea ofisi za ITV.

# DC atangazia vita wanaoficha mafataki

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKUU wa Wilaya ya Muheza, Halima Bulembo, amewaonya wazazi wanaowaficha na kushiriki kuwatorosha wanaume wanaowapa ujauzito wanafunzi na kuwataka kuacha mara moja.

Amesema vitendo hivyo ambavyo vinaendelea kushamiri katika maeneo mbalimbali nchini, vinakatisha ndoto za wasichana za kuendelea na masomo.

Bulembo alitoa onyo hilo juzi wakati akizungumza wananchi kwa nyakati tofauti kwenye mikutano ya hadhara kwenye vijiji vya tarafa ya Amani.

Alisema serikali kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ambayo yeye ni mwenyekiti, imejipanga kuwasaka wazazi wenye tabia hizo ili wakibainika wachukuliwe hatua kali kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa Bulembo, kumeibuka tabia kwa baadhi ya wazazi, watoto wao wa kike wanapopewa ujauzito na wanaume, wanakubali kuzungumzia suala hilo nyumbani na kukubali kupokea ng'ombe na vitu kadhaa wakati ambao tayari ndoto za mtoto wao zimeshavunjwa.

Bulembo alisema kamwe serikali haitawavumilia wazazi wa aina hiyo wanaowafanya watoto wa kike kama kitega uchumi cha kupata fedha wakati bado wanasoma.

Alisema wazazi wanapoona mtoto amepewa mimba wanatakiwa kutoa ushirikiano kwa serikali ili mhalifu akamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria badala ya kumsaidia atoroke na kwamba akitoroka ni bora mzazi naye afanye hivyo vinginevyo atakumbana na mkono wa sheria.

"Ukiona mtoto au mhalifu amekimbia na wewe kimbia maana tukikukuta tunakukamata," alisema.

Bulembo alisema tabia ya wazazi kuficha wahalifu ambao wanawakatiza ndoto za wasichana inazidi kuota mizizi.

Aidha, aliwalaani wanaume ambao wana tabia ya kuwarubuni wasichana wadogo wa shule na kuwapa ujauzito.

Muswada wa pili wa marekebisho ya sheria mbalimbali wa mwaka 2016 kuhusu elimu, umetoa adhabu kwa anayempa ujauzito mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari, kuoa au kuolewa na mwanafunzi na mwanafunzi kuoa mtu yeyote, kuwa ni kifungo cha miaka 30 jela na faini ya Sh. milioni tano.



Mkurugenzi wa Uhusiano, Mawasiliano na Sheria wa TBL, Mesiya Mwangoka, akieleza mkakati wa kampuni kufanikisha kampeni za usalama kwa maofisa waandamizi wa polisi kutoka kikosi cha usalama barabarani katika mkutano kuhusu masuala ya usalama barabarani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maeneo 20 yatangazwa kung'arisha usafi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Nipe Fagio, inayohusisha jamii, sekta binafsi na serikali katika kufikia maendeleo endelevu juu ya udhibiti wa taka, imeyatangaza rasmi maeneo ya usafi kuelekea Siku ya Usafi Duniani kwa mwaka 2021.

Siku ya Usafi Duniani kwa Tanzania inatarajiwa kusherehekewa ndani ya siku mbili ambazo ni Septemba 11 na 18, na imepangwa kufanyika katika maeneo 20 mkoani Dar es Salaam na mengine 20 katika mikoa mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Nipe Fagio, Ana Rocha, alisema shughuli hiyo itafanyika katika maeneo hayo kwa kushirikiana na taasisi ambazo wamekuwa wakishirikiana nazo kwa muda mrefu sasa.

"Malengo ya kuandaa usafi huu kwenye maeneo haya ni kuwawezesha watu kuwa na ufahamu wa uchafuzi wa taka unaofanyika nchi nzima na kukusanya takwimu na kuchochea utatuzi ufanyike kama uwajibikaji kwa mzalishaji, ambao utatatua changamoto hii," alisema.

Kutokana na uwepo wa janga la corona, alisema Nipe Fagio ilizimika maeneo haya ya usafi kugawanywa katika tarehe tofauti ikiwa katika lengo la kugawanya maudhurio na kupunguza idadi katika eneo moja la usafi.

"Tumeamua kugawanya usafi katika siku mbili kwa kuwa hili litasaidia kupunguza idadi ya washiriki kwa kila eneo. Tahadhari zote zitachukuliwa kukiwa na vituo vya kuoshea mikono. Tunasisitiza sana kwa mtu yeyote atakayeshiriki usafi huu kuja akiwa amevaa barakoa," alisema.

Aliyataja maeneo ambayo usafi huo utafanyika kuwa ni Bariadi (Simiyu), Iringa, Korogwe (Tanga), Mafia, Mbeya, Moshi, Mwanza, Njombe, Rukwa, Shinyanga, Zanzibar, Bukoba, Kipili (Ziwa Tanganyika) na Dar es Salaam.

Ikiwa taasisi mwongozaji wa Siku ya Usafi Duniani nchini Tanzania, alisema Nipe Fagio inategemea kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwenye makundi mbalimbali ya jamii, watu wanaojitolea na wadau wengine katika sekta ya mazingira katika kuifanya hii Siku ya Usafi Duniani kuwa ya kipekee na yenye mafanikio zaidi.

"Tunahitaji kufanya kazi pamoja tukiwa na lengo moja la kushinda uchafuzi wa mazingira utokanao na plastiki na kuifanya Tanzania kuwa nchi safi na yenye afya nzuri kupitia kukuza uelewa, ukusanyaji takwimu na kuchochea mabadiliko chanya," alisema mkurugenzi huyo.

## 'Bila mafunzo hakuna ajira'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, amesema fursa za ajira zitakazotolewa katika wilaya hiyo kipaumbele kitakuwa kwa waliopitia mafuzo ya jeshi la akiba.

Msafiri alibainisha hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya awali ya jeshi la akiba kwa vijana 75 yanayofanyika katika kata ya Kwala. Alisema nafasi za kazi zipo kwa vijana wazalendo ambao wako tayari kuilinda nchi yao.

"Kibaha hatapelekwa mtu Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wala kupata kazi bila kupitia mafunzo ya mgambo," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa vijana hao kuangalia kazi za kufanya za kujiajiri baada ya kuhitimu mafunzo hayo.

Aliwaelekeza kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ambavyo vitapatiwa mikopo.

Msafiri alisisitiza vijana kuwa na nidhamu kuwa waadilifu kwa kulinda rasilimali za nchi ikiwamo miundombinu ya miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa.

Mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya ya Kibaha, Meja Mohamed Khamis, alisema mafunzo hayo ya miezi minne yanalenga kusogeza huduma ya ulinzi karibu na wananchi.

Alisema lengo lingine la mafunzo hayo ni kulinda maeneo nyeti wakati wa amani na wakati wa vita lakini pia kusaidia Polisi kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, Sophia Ramadhani na Juma Said, walisema mafunzo hayo yatawawezesha kuwa imara kuilinda nchi yao kuwa wazalendo katika suala la ulinzi na usalama.

## Washindi kampeni NMB kupaa Dubai

**Na Beatrice Moses**

BENKI ya NMB imezindua kampeni ya 'NMB Kama Upepo,' iliyotokana na makubaliano ya kibiashara na Kampuni ya Skylink Travel & Tours, inayojihusisha na uwakala wa tiketi za ndege.

Kampeni hiyo itakayowazawadia washindi sita na wenza wao safari iliyolipiwa gharama zote kwa siku tatu nchini Dubai.

'NMB Kama Upepo' ni kampeni itakayoendeshwa kwa miezi mitano, ikilenga kuchagiza matumizi ya kadi za NMB MasterCard na QR Code miongoni mwa wateja wa benki hiyo kwa ajili ya kununua tiketi za ndege, ambako watapata punguzo la asilimia 60 ya ada ya huduma.

Akizungumza wakati wa uzinduzi jijini Dar es Salaam, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, alisema kampeni hiyo itakuwa na zawadi za kila wiki na kila mwezi kwa wateja wa NMB watakaofanya malipo ya tiketi za ndege kutoka Skylink kwa kutumia MasterCard na QR Code.

"Kadri mteja atakavyotumia kadi katika manunuzi ya mitandaoni au kufanya malipo kupitia kadi za NMB kwenye tovuti ya Skylink, ama mashine zetu za malipo (POS) zilizoko katika ofisi za washirika wetu hawa, ndivyo atavyojiongezea nafasi za kushinda zawadi kutoka kwetu.

"Katika kipindi chote cha kampeni hii ya NMB Kama Upepo, inayoanza Septemba 1, 2021 hadi Januari 2022, washindi sita na wenza wao (jumla watu 12), tutawazawadia safari iliyolipiwa gharama zote, ikiwamo malazi kwa siku tatu huko Dubai, tiketi za ndege za kwenda huko na kurudi nchini, pamoja na pesa za matumizi," alisema Mponzi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Skylink, Moustafa Khataw, alisema Skylink ina furaha kubwa sio tu kuingia makubaliano ya kibiashara na NMB, bali pia kuwa sehemu ya Kampeni ya NMB Kama Upepo, na kwamba wateja wa benki hiyo watafurahia huduma chanya zinazoenda kutolewa katika miezi yote ya uwapo wake.

"Tuna furaha kufanikisha makubaliano haya, yanayoenda sambamba na uzinduzi wa NMB Kama Upepo. Tunaishukuru Menejimenti ya NMB kwa ushirikiano huu na ahadi yetu kwa wateja wa benki hiyo ni kuwahakikishia huduma bora, nafuu, salama na rahisi ya manunuzi ya tiketi," alisema Khataw.

# Wadai zahanati haina sifa kuhudumia wanaojifungua

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAJAWAZITO katika Kata ya Kalela Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma wanapeana zamu kulazwa kitandani kujifungua na wengine kulazwa chini, kutokana na Zahanati ya Kalela kuwa na chumba kimoja cha wodi ya wazazi chenye kitanda kimoja tu.

Editha Ramadhani, mama mwenye mtoto mdogo ambaye amejifungua hivi karibuni, alisema kitendo cha kulazwa kitandani kwa zamu na wengine kulazwa chini wakati wakiwa na uchungu si jambo la kupendeza na wanaliona lina hatarisha katika usalama wa mama na mtoto.

Pia Editha ameiomba serikali iboreshe miundombinu ya zahanati hiyo ikiwamo kuongeza wodi ya wazazi na vitanda, hatua itakayosaidia uzazi salama.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Njela Nikasi, alieleza upungufu huo unasababisha adha kubwa kwa wajawazito na kuomba hatua za haraka kukabiliana nalo.

"Wajawazito wakiwa zaidi ya mmoja wanachukua aliye karibia kujifungua anawekwa kitandani wengine wanalazwa chini, huyo wa kitandani akichelewa anashushwa chini, ili mwingine alazwe kitandani kujifungua."

Diwani wa Kata ya Kalela, Deogratius Kabigwa, alisema anatambua uwapo wa tatizo hilo linalosababisha wajawazito kupeana zamu kulazwa kitandani na wengine chini.

Akitoa ufafanuzi juu ya madai hayo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Dk. Robert Rwebangira, alisema katika zahanati hiyo kwa mwezi wanajifungua wanawake 33 hadi 35 sawa na wastani wa mwanamke mmoja kwa siku.

"Lazima tutumie takwimu zilizopo, sisi takwimu zetu hazi refrect (haziakisi) hivyo, kwani kwa mwezi wanazalisha wanawake 33 hadi 35 labda kuwe na takwimu zingine ambazo sisi hatuzifahamu," alisema Dk. Rwebangira.

Alisema hata uwanja wa mpira kuna siku unajaa, hivyo huwezi kujenga mwingine kwa sababu kuna siku umejaa, lakini kutokana na takwimu hizo zahanati hiyo bado inakidhi vigezo.




Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto (kulia), akipokea ripoti ya utendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) kwa mwaka 2020 kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alipofanya ziara ya kikazi katika makao makuu ya TCB, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magonjwa sugu yatafutiwa mwarobaini

**Na Christina Mwakangale**

KWA mara ya kwanza, Chama cha Watafiti na Wataaluma wa Vinasaba vya Binadamu Tanzania (THGO) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, wanafanya utafiti kwa makabila kadhaa kutoka kanda tofauti nchini, kubaini asili ya magonjwa sugu, yasiyoambukiza ili kupata tiba na chanjo sahihi inayofaa.

Makamu wa Rais wa THGO, Dk. Kilaza Samson, amesema utafiti huo utalenga makabila makubwa ambayo yatawakilisha mengine ikizingatiwa Tanzania inayo takribani 120.

Dk. Samson aliyasema hayo jijini Dar es Salaam kwenye mkutano na waandishi wa habari kuhusu mkutano wa 13 wa kimataifa ulioanza jana kukutanisha wanataaluma wa vinasaba na chembechembe za urithi kwa binadamu 200 kutoka taasisi za serikali, binafsi na wadau wengine kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema utafiti huo utaanza hivi karibuni na awali itatolewa elimu kwenye maeneo ambako utafanyika na kwamba utasaidia kubaini familia na maeneo yaliyo na magonjwa sugu ikiwamo kisukari, presha, selimundu na saratani wanahitaji tiba gani na namna ya kuvikinga vizazi vyao mapema.

"Ni muhimu kujua kiini cha magonjwa na namna ya kuwapa tiba sahihi wagonjwa hata chanjo. Taasisi za tiba baada ya utafiti huu itakuwa rahisi kubuni dawa ambazo zitalenga eneo fulani kulingana na mazingira na vinasaba vyao," alisema Dk. Samson.

Alisema takwimu hizo zitasajiliwa na kutunzwa kwa matumizi ya kitabibu ambayo hivi sasa nchi zilizoendelea hutumia teknolojia inayojihusisha na vinasaba kubaini magonjwa, kubuni dawa na chanjo zinazolingana na mazingira yao.

Mtaalamu wa Vinasaba kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Ally, Kanenda, alisema ofisi hiyo imekuwa ikitumia teknolojia hiyo husuan kwa kesi za jinai, migogoro na kubaini jinsi tata.

"Katika jinsi tata inarahisisha madaktari kuamua wanaozaliwa na jinsi tata wafanyiwe tiba na kubaki na jinsi moja. Tutashirikiana katika utafiti huu na chama hiki ili kupata kanzidata ambayo haipo nchini," alisema Kanenda.

Rais wa chama hicho, Dk. Siana Nkya, alisema kupatikana kwa kanzidata hiyo kutasaidia kupata chanjo ya magonjwa mbalimbali ambayo inaendana na vinasaba ya mwafrika na kwamba mkutano wa leo unawaleta pamoja wanazuoni wachanga na wabobezi kujadili namna ya kuboresha matibabu.

Prof. Raphael Sangeda, kutoka Chuo cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), alisema wakati kipindi hiki kuna ugonjwa wa Covid-19 na chanjo kuanza kutolewa, kumeibuka taharuki kwa baadhi ya jamii wakidai chanjo si salama.

"Vinasaba vikijulikana itajulikana familia hii hurithi magonjwa haya, tiba ni ipi muafaka hata tutajua wanaougua magonjwa adimu watibiwaje," alisema Prof. Sangeda.

# Askari wa Zimamoto sasa kutumia silaha

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni muswada ili kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura ya 427 kwa lengo la kuondoa upungufu uliobainika katika sheria hiyo wakati wa utekelezaji wake.

Miongoni mwa marekebisho yanayotarajiwa kufanyika ni kuongeza kifungu kipya cha 11A ili kuwapa askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji haki ya kutumia silaha wakati wa utekelezaji wa majukumu, wajibu na mamlaka yao yaliyoainishwa chini ya sheria.

Muswada huo uliosomwa kwa mara ya kwanza bungeni jijini Dodoma jana, unabainisha kuwa lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha usalama wa miundombinu ya jeshi, maofisa na askari.

"Marekebisho pia yanapendekezwa katika kifungu cha 13 kwa kuongeza adhabu ili iendane na wakati na hivyo kuzuia utendaji wa makosa. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utendaji wa makosa yaliyoainishwa katika sheria.

"Kifungu cha 22 kinarekebishwa kwa kumtaka mmiliki au msimamizi wa jengo kufunga mfumo wa vifaa vya moto kwenye jengo hilo.

"Vilevile, marekebisho katika kifungu hiki yanaweka sharti kwa mtu yeyote anayekusudia kujenga jengo lenye urefu wa kuanzia mita 12 kutoka usawa wa ardhi, kuwasilisha mchoro wa ujenzi wa jengo kwa Jeshi la Zimamoto kwa ajili ya ukaguzi na ushauri wa kiusalama kuhusu masuala ya moto kabla ya kuanza kwa shughuli za ujenzi," inabainisha katika muswada huo.

Pia marekebisho yanapendekezwa kufanyika katika kifungu cha 27 kwa kutoa fidia kwa askari wa Jeshi la Zimamoto na watu wanaojitolea ambao hujeruhiwa au kufariki dunia wakati wa kupambana dhidi ya majanga ya moto.

Muswada pia unapendekeza marekebisho katika sheria kwa kuongeza vifungu vya 31A na 31B kwa kuweka adhabu ya jumla na ufikilishaji wa makosa.

Lengo la marekebisho hayo ni kuboresha utaratibu wa utoaji adhabu na kupunguza mlolongo mrefu wa mashauri mahakamani. Vilevile, kifungu cha 32 kinarekebishwa ili kuongeza wigo wa maeneo ambayo waziri anaweza kutunga kanuni ili kuzisimamia kampuni binafsi saidizi zinazotoa huduma za zimamoto na uokoaji.

Sehemu ya tatu ya muswada huo inapendekeza marekebisho yatokanayo katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza (Sura ya 241) na Sheria ya Ajira na Uhusiano wa Kazi (Sura ya 366), kwa kuboresha tafsiri mbalimbali katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza ili ziendane na marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Vilevile marekebisho katika sheria hii yanakusudia kujumuisha wajumbe kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwenda Tume. Aidha, Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, Sura ya 366 inarekebishwa kwa lengo la kulijumuisha Jeshi la Zimamoto katika orodha ambayo masharti ya Sheria ya Ajira na Uhusiano wa Kazi hayatatumika.




Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara cha Vodacom Tanzania, Arjun Dhilon (kushoto), akizungumza na wajasiriamali wanawake wakati wa maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali, jijini Dar es Salaam jana, wenye lengo la kukuza biashara zao kupitia kampeni ya kampuni hiyo ya 'Pamoja Tukuze Biashara Yako' iliyo chini ya muunganiko wa kidunia wa 'SheMeans-Business'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wa elimu watakiwa kutembelea vituo vya urithi

**Na Ally Mlanzi-** TUDARCO

WIZARA ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kupitia programu ya urithi wa ukombozi wa Afrika, imewaomba walimu wa sekondari na shule za msingi pamoja na wadau wwa elimu kutembelea vituo vya urithi wa ukombozi vilivyopo nchini, ili kuweza kupata maarifa.

Rai hiyo ilitolewa jana na Ofisa Utamaduni wa wizara hiyo, Christopher Mhongore, wakati wa mahojiano na Nipashe kuhusu dira ya programu hiyo.

Alisema vituo vya urithi wa ukombozi vipo maeneo mbalimbali nchini ikiwamo mkoani Dodoma, Lindi na Dar es Salaam.

Mhongore alisema: "Kama walimu na wadau wengine watakua na tabia ya kuleta vijana wao au wenyewe kuja kujifunza itasaidia sana kuijulisha jamii juu ya urithi wa ukombozi na kuendeleza utalii wa urithi wa ukombozi."

Alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni kukosa wadau ambao watasaidia kuijulisha jamii juu ya urithi wa ukombozi kama vile walimu na wanafunzi waliopo vyuoni.

Alieleza wizara ipo tayari kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha urithi unamfikia kila mtu, kwani licha ya kuwa ni sehemu ya utalii lakini utaifanya jamii ione umuhimu wakudumisha amani na mshikamano, kulinda na kupigania nchi kwa uzalendo.

Aidha, alisema dhamira yao kuu ni kuhakikisha kuwa urithi wa Afrika unatambuliwa, unahifadhiwa, unalindwa na kutangazwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika.

# ACB kuwafikia watu 100,000 miezi 3 ijayo

**Na Enock Charles**

BENKI ya Biashara ya Akiba Plc (ACB) inatarajia kuwafikia zaidi ya wateja 100,000 wake na wasio wateja wake katika katika kipindi cha miezi mitatu ijayo kupitia huduma yake ya Akiba Wakala.

Dora Saria, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa ndani ya wiki tatu za kwanza tangu huduma hiyo ianzishwe sokoni, imevutia maelfu ya watumiaji.

"Tunatarajia kuwafikia wateja zaidi ya 100,000 wa Akiba Wakala kwa wateja na wasio wateja. Kuchukuliwa kwa huduma hiyo imekuwa ya kushangaza machoni mwa watumiaji tangu kuanzishwa kwake karibu wiki tatu zilizopita;

Tumekuwa tukipokea maombi kadhaa ya kuanzisha maduka ya Akiba Wakala kutoka maeneo tofauti nchini ambapo huduma bado hazijatolewa. Hii inaonyesha kuwa huduma imekuwa ya kuvutia kwa umma kwa ujumla," alisema Saria.

Katika kuongeza ufanisi wa benki hiyo, alisema ipo mbioni kufungua ukurasa mpya wa kibiashara kwa kujenga mfumo thabidi wa utoaji huduma kidijitali baada ya kupata mwekezaji wa kimkakati ambaye ni Benki ya Taifa ya Malawi (NBM).

Ubia huo kati ya ACB na NBM uliofikiwa hivi karibuni, unalenga kuijenga zaidi benki hiyo kwa kutanua mtandao wake wa kuduma za kifedha hapa nchini na kuhimili ushindani miongoni mwa watoa huduma. Ubia huo ni wa muda mrefu na tayari umeshaanza kuonesha matunda kama vile kuanzishwa kwa huduma ya Akiba Wakala.

"Benki imepata mwekezaji wa kimkakati, ambaye ni NBM. Tuna imani kwamba ubia huu utasaidia kupanua wigo wetu wa kibiashara ikizingatiwa NBM ni moja ya benki kubwa kwenye ukanda wetu wa nchi za kusini mwa Afrika;

"Ushirikiano tulioanzisha kati yetu na NMB umeleta ari kubwa ambayo siyo tu ya kuhakikisha huduma za benki zinapatikana nchi nzima bali zinapatikana kidijitali na kwa uhakika," alisema Saria.

Alisema mchakato wa kuibadili benki kuwa ya kidigitali unaendelea vizuri na tunauhakika utaleta unafuu na kuokoa gharama za upatikanaji wa huduma.

Kwa sasa benki inatoa huduma ya Akiba Mobile, ambayo inawezesha wateja wake kufanya malipo ya LUKU, ving'amuzi, muda wa maongezi pamoja na malipo yote ya serikali.

Akiba Mobile pia inapatikana kupitia mfumo wa USSD. Inamwezesha mteja kufanya miamala yake ya kibenki kupitia mawakala pia. Benki inatoa huduma nyingine za amana, mikopo, kuuza na kununua float, kutuma na kupokea fedha kupitia Western Union.

Alisema Benki ya Akiba siku zote imekuwa mstari wa mbele katika kufanya utafiti mbalimbali wa kuangalia mahitaji ya soko na wateja wake kwa ujumla, kwani inatambua umuhimu wa kutoa huduma zinazoendana na mahitaji ya soko.

Akizungumzia huduma ya Akiba Wakala ambayo imeanza kutolewa takribani wiki tatu sasa, Saria alisema tayari imeanza kutoa matokeo mazuri kwa kuwezesha wateja kupata huduma kwa urahisi zaidi popote pale walipo.


"Tunaamini kwamba kupitia huduma hii benki inakuwa mshiriki mzuri katika kuunga mkono harakati za serikali za kuhakikisha uwapo wa huduma jumuishi za kifedha yaani kwa Watanzania wote.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 2, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## Ni kilio, watoto bilioni 1 hatarini athari mabadiliko ya tabianchi



Ukurasa 13

## UVIKO-19 unavyoitesa sekta ya madini

# Wanakijiji hawa wanapolizwa na mengi...

## •Kukosa usingizi, kuchangia maji na mifugo, wanyama pori



Wakazi wa Kijiji cha Kilololi, Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, wakisubri maji kwenye bwawa la kijiji hicho ambalo limeanza kukauka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

KWA wanakijiji cha Kiloleli ni kawaida kuondoka nyumbani kila siku saa 2:00 usiku na kurejea kesho yake asubuhi baada ya kutembea zaidi ya kilomita 15 ili kuchota maji katika kijiji kingine kwa vile hakijawahi kuwa na majisafi na salama ya bomba au kisima."

Ni ushuhuda wa Kwangu Limbu, mkazi wa kijiji hicho, kilichoko wilayani Kishapu mkoa wa Shinyanga, anayesema tangu operesheni vijiji ya mwaka 1974 hajawahi kuona maji ya bomba.

Kwangu anaiambia Nipashe anayasema kuwa kwa kutambua umuhimu wa bajeti ya mrengo wa kijinsia upande wa maji, iliyofanyika hivi karibuni Dar es Salaam, ikishirikisha wadau kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Katika maelezo yake, anasema, wakazi wa kijiji hicho hufuata maji usiku katika bwawa la Manonga lililochimbwa katika Kijiji cha Manonga.

"Tunafanya hivyo usiku kwa sababu mchana ni zamu ya wafugaji kunywesha mifugo yao. Tunalazimika kwenda usiku, kwa sababu bwawa hilo tunachangia binadamu, mifugo na wanyama pori...," anasema Kwangu.

Akifafanua zaidi kuhusu safari ya kwenda kufuata maji, anasema hutumia mikokoteni ya kukokotwa na ng'ombe ambayo watu huweka mapima na kuanza safari ambayo wanarejea kesho kuanzia saa 2:00 asubuhi.

"Hali hiyo inakwamisha shughuli nyingine za maendeleo, lakini tufanyeje, kwa sababu maji ni uhai, hivyo ni muhimu tuwe nayo japo ya siku mbili kisha tunakwenda tena usiku kuyafuata," anasema.

**MRENGO WA KIJINSIA**

Mchambuzi wa masuala la kijinsia ambaye alikuwa mwezeshaji wa mafunzo hayo, yanayoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) Deogratius Temba, anasema umuhimu wa bajeti ya mrengo wa kijinsia unagusa maeneo mengi.

Kwa mfano, watu wanaotafuta maji ni wanawake, lakini kama miaka yote bejeti zingezingatia mrengo wa kijinsia, huduma mbalimbali kama maji zingepatikana maeneo ya karibu ili kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu," anasema Temba.

Aidha, ukosefu wa maji unaweza kusababisha kinamama kupoteza muda katika kuhangaikia huduma hiyo huku kazi nyingine zikilala na pia wanafunzi wasichana kuchelewa vipindi shuleni.

"Mtu anaondoka saa 2:00 usiku kufuata maji anarudi kesho asubuhi, anaweza kufanya shughuli nyingine za maendeleo akiwa na usingizi? Hii inaonyesha bado tuna safari ndefu kufikia bajeti ya mrengo wa kijinsia," anasema Temba.

MIMBA na NDOA ZA UTOTONI

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiloleli, Kuhwema Mashala, anasema tatizo hilo la ukosefu wa maji linaongeza shida nyingine ya mimba na ndoa za utotoni suala lililo hatari kiafya.

"Sina idadi kamili ya mimba na ndoa za utotoni, lakini ukweli ni kwamba safari za kufuata maji zinasababisha tatizo hilo, kwani wapo baadhi ya watu wanaorubuni mabinti wanapokutana huko usiku," anasema Mashala.

Anafafanua kuwa kijiji hicho kilianzishwa mwaka 1974, kina kaya 600, na kwamba tangu kianzishwe, hakina chanzo cha uhakika cha maji, hali ambayo husababisha wakazi wake kusafiri umbali mrefu kuafua huduma hiyo.

Mwenyekiti huyo anasema, kijiji hicho kina bwawa ambalo wananchi hutumia maji yake kwa miezi michache kisha hukauka na kusabaabisha wasafiri umbali mrefu wakati wa usiku hadi Manonga.

"Bwawa linajaa maji wakati wa masika, na kiangazi limekauka, wakazi wa kijiji changu wameanza safari za usiku ya kwenda hadi Manonga, haya ni mateso...," anasema.

anaongeza kuwa mazingira hayo yanaumiza, hasa watu kusafiri usiku kufuata maji, kuwapo kwa mimba na ndoa za utotoni ambazo zinawaweka mabinti katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya ngono kukatishwa masomo.

**ATHARI KUCHANGIA MAJI**

Mtaalamu wa afya anaeleza kuwa kuna athari mbalimbali za kiafya ambazo mtu anaweza kuzipata iwapo atachangia maji na wanyama wakiwamo wa kufugwa au wa porini.

Dokta Madiwa Madiwa wa Kituo cha Afya Sinza Palestina, anataja baadhi ya athari hizo kuwa ni kupata magonjwa mbalimbali kama kichocho, kipindupindu, kuharisha, homa ya tumbo. Minyoo na

INAENDELEA UK.12

AFYA

## KINAMAMA VS U.T.I SUGU

# Uchafu, kushindwa kunawa kikamilifu mwanzo U.T.I sugu



Kuwahi hospitalini na kutumia dawa kikamilifu ni mbinu ya kupunguza makali ya U.T.I sugu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Donald Lukele, TUDARCo**

MAAMBUKIZI sugu ya njia ya mkojo au U.T.I ni ugonjwa unaotesa wengi hasa wanawake, aidha kukosa elimu ya kina juu ya maradhi hayo, kumesababisha watu kuishi na maambukizi hayo bila kujua ni namna gani na ni njia zipi za kuyaepuka.

Umewahi kukijua kinachosababisha U.T.I sugu inayojirudia rudia? Je, ni kundi gani huathirika zaidi na ugonjwa huo na ni jinsi gani ya kuuepukana? Dk. Johnson Joseph, kutoka Hospitali ya Rufani ya KCMC mkoani Kilimanjaro, anayo maelezo.

Anasema kuwa maambukizo yanayoendelea kwa muda mrefu licha ya kupata matibabu sahihi ndiyo yanayoitwa U.T.I sugu, akifafanua kuwa wanawake ni waathirika wa ugonjwa huo kutokana na kushindwa kuzingatia usafi kamili na hivyo kujiambukiza wenyewe kila wakati na kuishi na tatizo hilo hatari.

Anaeleza kuwa vimelea au bakteria wanaoambukiza ugonjwa huo wanaweza kujishikiza kwenye njia za mkojo hivyo kuwa sugu na kutotibika na kuendelea kurudia mara kwa mara na kushambulia.

Dokta Joseph anaeleza kuwa kutomaliza dozi ya kutibu ugonjwa au kutozingatia muda sahihi wa matumizi ya dawa huleta usugu wa bakteria hao wanaoshambulia mfumo wa mkojo.

"Kwa maana hiyo ni muhimu kujua ni nini chanzo cha usugu wa ugonjwa huo kwa mgojwa ili kujua ni jinsi gani aweze kupata tiba sahihi."

**CHANZO CHA MARADHI**

Anasema kinachosababisha tatizo hilo maambukizo katika mfumo wa mkojo, baada ya kushambuliwa na vimelea kama bakteria, fangasi na virusi.

"Usugu unatokana na kujirudia hata baada ya mgonjwa kutibiwa," anasema mtaalamu huyo na kuongeza kuwa mara nyingi bakteria wanaoingia kwenye mfumo wa mkojo huondolewa na mifumo ya mwili, wenyewe lakini wakati mwingine wanaweza kuizidi nguvu kinga ya mwili na husababisha maambukizo."

Anasema watu wote wapo katika hatari ya maambukizo sugu ya mfumo wa mkojo lakini wanawake wana hatari zaidi kwa sababu, mfumo wa mkojo wa mwanamke au njia yao ya mkojo ipo karibu na eneo la haja kubwa hivyo ni rahisi bakteria kutoka katika eneo hilo na kufika katika sehemu za siri za mwanamke hasa wakati anapojisafisha.

Anakumbusha kuwa unapojisafisha baada ya haja ni vyema kusafisha sehemu ya haja ndogo kwanza, kisha eneo la haja kubwa na kuepuka kutoa uchafu (choo) nyuma na kuiweka sehemu za siri.

Anasema kama unatumia karatasi laini anza kujifuta kutoka mbele kwenda nyuma na siyo nyuma kwenda mbele, utakuwa umejipaka choo ambacho kina wadudu wanaoeneza U.T.I.

Anashauri kwa wanawake kufanya hivyo wanapojisafisha na pia kusafisha watoto wa kike na kuanza kumfuta mtoto kuanzia mbele kwenda nyuma kwenda kwenye haja kubwa na siyo kufuta haja kubwa na kutumia karatasi hilo kumfuta sehemu za haja ndogo.

"Pia njia ya mkojo ya mwanamke ni fupi kuliko ya mwanaume. Kwa sababu hii bakteria huwa na umbali mfupi wa kusafiri kufika kwenye kibofu cha mkojo." Anakumbusha na kuhimiza usafi.

**MADHARA UTI SUGU**

Dokta Joseph anasema usugu ni hatua mbaya kwani kawaida huingia kwenye njia ya mkojo kupitia bomba linalobeba mkojo kutoka kwenye figo hadi kibofu cha mkojo.

"Ikiwa maambukizo huanza kwenye mkojo na kibofu huweza kudhibitiwa kwa matabibu, walakini ikiwa UTI itafika kwenye figo inaweza kuwa mbaya zaidi hivyo nawashauri watu wanaosumbuliwa na ugonjwa huu kufika vituo vya afya mapema kupata matibabu kabla ya madhara hayajawa makubwa," anasema Dk. Joseph.

Mkojo wa mwenye UTI unakuwa na harufu mbaya na hata kubadilika rangi kuwa wa njano iliyo iva au mawingu wengi huchukulia ni swala la kawaida bila kufahamu mfumo wao wa mkojo una mambukizi.

"Aliyeathiriwa na ugojwa huu hupata maumivu mgongoni au kwenye mbavu hasa upande mmoja, na kutapika wengi hapa huhisi ni malaria au homa ya tumbo, kuhisi maumivu ya misuli na tumbo pia ni dalili.

**KUJIKINGA U.T.I SUGU**

Njia ya kwanza ya kujikinga ni kufika kituo cha afya pale unapoona una tatizo na kupata matibabu kamili na pia kutumia dozi kwa usahihi kwani wengi hujikuta wakipata usugu wa ugonjwa huo, kutokana na kutomaliza dozi.

Kunywa maji mengi kwa siku takriban lita moja na nusu au zaidi ili kusafisha njia ya mkojo na kujiweka salama na magonjwa mbalimbali, lakini kuzingatia usafi katika sehemu za siri kwa kuvaa nguo za ndani zilizo safi na kujisafisha kwa utaratibu wa kuanzia mbele kurudi nyuma wanawake ni mambo ya kuzingatia.

Anashauri mtu anapohisi kujisaidia haja ndogo asijibane. Kuzuia mkojo husababisha maambukizo ya U.T.I kwani mkojo ukikaa kwa muda mrefu kwenye kibofu huzalisha bacteria, anasema Dk. Joseph..

Anatahadharisha kuacha kufanya ngono kinyume na maumbile kwani ni sababu moja wapo ya kupata magonjwa mengi ya mfumo wa mkojo hususan U.T.I

Anawashauri watu kuepuka kuvaa nguo zinazobana kupita kiasi ili kuruhusu hewa kupita katika sehemu za siri ni njia salama ya kujiepusha na ugonjwa huo.

Anashauri pia kuwa msafi, kunawa na kuvaa nguo za ndani zilizokauka kikamilifu ili kuepusha kukua kwa vimelea vinavyoleta magonjwa hayo.

# Wanakijiji hawa wanapolizwa na mengi...

**INATOKA UK.11**

Kifua Kikuu TB.

"Kwa kawaida wanyama hunywa na maji na kujisaidia humo, na ikumbukwe kuwa vinyesi vyao vina magonjwa mbalimbali, ndiyo maana watumiaji wa maji hayo wanaweza kukumbwa na magonjwa," anasema.

Anasema kutokana na tatizo hilo, njia nzuri inayoweza kusaidia kuendelea kutumia maji pamoja na wanyama ni kuweka mpangilio wa kugawa sehemu tatu ukiwamo ya kuchota maji ya kutumia nyumbani, sehemu ya kufulia na ya mifugo.

Anafafanua kuwa sehemu ya kuchota maji ya kutumia nyumbani inaweza kuwa ya mwinuko, ikafuatia ya kati ambayo kwa ajili ya watu kufua na nyingine ya chini ambayo itatumiwa na wanyama kunywa maji.

**MRADI MKUBWA WA MAJI**

Mbunge wa Kishapu, Boniface Butodo, ambayo kijiji hicho kipo katika jimbo lake, anakiri kuwapo kwa tatizo la maji, na kusema kuna mradi wa maji kutoka ziwa Victoria ambao ana uhakika utamaliza tatizo la Kiloleli.

"Serikali imetenga zaidi ya Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya mradi huo, umeshafika katika baadhi ya kata jimboni mwetu, ninadhani kufikia mwaka 2015, wakazi wa Kiloleli watapata maji ya bomba kutoka ziwa Victoria," anasema Butondo na kuwatoa wasiwasi.

Mbunge huyo anafafanua kuwa mbali na kusubiri mradi wa maji wa Ziwa Victoria, kuna mkakati wa kupanua na kuongeza kina cha bwawa la kijiji hicho ili maji yapatikane kwa wingi na kwa muda mrefu.

"Tukipanua na kuongeza kina, tunaweza kuwa na unafuu wa upatikanaji wa maji, lakini kwa sasa bwana limejaa tope, hali ambayo inalazimisha wakazi wa kijiji hicho kwenda kwenye chanzo, mto Manonga," anasema.

Aidha, mbunge huyo anatofautiana na wakazi wa kijiji hicho na mwenyekiti kuhusu umbali wa kutoka Kiloleli hadi Manonga, kwamba ni umbali wa kilomita tano na siyo 15 kama wanavyoeleza.

"Lakini si kwamba kuna bwawa lililochimbwa na wafugaji, bali ni eneo la chanzo cha maji ya Mto Manonga ambacho maji yake hayakauki kama ilivyo kwenye bwawa la Kiloleli," anasema.

**BAJETI YA MAJI 2021/2022**

Wizara ya Maji inatarajia kutumia Shilingi bilioni 680.3 katika bajeti ya mwaka 2021/2022, huku Waziri wa Wizara hiyo, Jumaa Aweso, akitaja mafanikio yaliyopatikana kuwa ni pamoja na ongezeko la huduma za maji nchini kutoka asilimia 70.1 vijijini na 84 mijini.

AFYA

# UVIKO-19 unavyoitesa sekta ya madini

## •Wafanyakazi waathirika kimaradhi, ajira

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MIGODI ya almasi ya Williamson Diamond na El Hilali yote iliyoko wilayani Kishapu Mkoa wa Shinyanga, haijaachwa salama na UVIKO-19, imelazimika kupunguza wafanyakazi na kusitisha uchimbaji madini. Yote hayo yakileta athari kwa mamia ya vijana wanaokosa kazi.

Mhandisi Mkuu wa Mgodi wa Mwadui, Shaghembe Mipawa, anasema Agosti mwaka jana, walisitisha uchimbaji madini, kutokana na soko lililoko Ubelgiji kushuka na kusababisha kuzalisha kwa hasara.

Mgodi huo uliogunduliwa mwaka 1940 na Dk. John Williamson, ulianza uchimbaji almasi kabla ya uhuru na kutoa ajira kwa watu wengi, kujenga miradi ya maendeleo kwenye vijiji jirani na mgodi huo pamoja na kuchangia mapato ya serikali.

Anasema, lakini kutokana uwapo wa UVIKO 19, shughuli za uchimbaji madini zilisimamishwa na kampuni kupunguza nusu ya wafanyakazi, lakini hakutaja idadi yao, huku akisema wengine wamekwenda likizo kwa malipo ya nusu mshahara.

"Licha ya soko la almasi kushuka duniani sababu ya corona, hata sisi wafanyakazi ndani ya mgodi tulipata maambukizo..."anasema Mipawa na kuongeza kuwa waliopunguzwa kufanya kazi ndani ya mgodi, kuna taratibu ambazo zinaendelea za kuwalipa stahiki zao."

Sinani Zahoro ni miongoni mwa wafanyakazi waliopunguzwa, anasema maisha yake kwa sasa ni magumu, kwa vile alitegemea ajira, ili kutunza familia yake ya watoto wawili na wategemezi watatu, huku akirusha lawama kwa uongozi wa kampuni kutowalipa stahili zao ipasavyo.

"UVIKO 19 imetuathiri sana tupo vijana wengi hatuna ajira na maisha yetu yalikuwa hapa Mwadui na tunapozungumza na wewe sasa hivi tupo tu nyumbani, hatuna kazi,"anasema Zahoro.

Tito Kuya naye alipunguzwa kazi katika mgodi wa EL Hilali, uliopo na ule wa Williamson Mwadui, anasema maisha yake kwa sasa ni magumu hana ajira, lakini hajalipwa stahiki zake kikiwamo kiinua mgongo.

"Tunamuomba Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Patrobas Katambi, anayeshughulikia masuala ya ajira atusaidie kupata stahiki zetu, sababu suala hili analijua na alishakuja hapa mgodini kuzungumza na wamiliki, tukaahidiwa kulipwa, lakini wako kimya,"anaongeza Kuya.



Mwenyekiti wa soko dogo la ununuzi wa almasi la Mji wa Maganzo, Mussa Senema, akimwelezea mwandishi wa gazeti hili, namna madini yalivyoadimika. **PICHA: MARCO MADUHU**

Mmoja wa wakandarasi kwenye mgodi wa Mwadui , Mbaru Kidiga, anasema wameathirika kiuchumi, malengo yao kuvurugwa, lakini hata mitambo imepata hitilafu kwa sababu ya kukaa muda mrefu, bila kufanya kazi.

"Corona imeathiri shughuli nyingi za kiuchumi, lakini kwasasa mgodi upo mbioni kuanza kazi na tumeanza kuandaa mitambo tayari kuingia kazini,"anasema Soud.

Pili Milembe ni mfanyabiashara wa bidhaa mbalimbali katika Mji wa Maganzo, eneo ambalo wafanyakazi wa Mwadui na Eli Hilali wanakwenda kupata mahitaji mbalimbali, anasema tangu kufungwa kwa migodi hiyo biashara imekuwa ngumu kwake.

"Mzunguko wa fedha sasa hivi umepungua sana kwenye mji wetu huu wa Maganzo, tangu migodi ilipositisha uzalishaji, hakuna tena muingiliano mkubwa wa watu kama ilivyokuwa hapo awali. Hali ni mbaya kweli,"anasema Milembe.

Mwenyekiti wa soko dogo la ununuzi wa almasi lililopo Mji wa Maganzo wilayani Kishapu, Mussa Senema, anasema wameathirika kiuchumi na kimaisha kutokana na kufungwa kwa mgodi wa Mwadui, sababu walikuwa wakinunua madini ndani ya mgodi huo na kuwainua kiuchumi.

Anasema licha ya wao kununua madini ya almasi kwa wachimbaji wadogo, lakini ununuzi wao mkubwa walikuwa wakitengemea madini kutoka ndani ya mgodi.

"Sasa hivi ununuzi wetu wa madini umebaki kwa hawa wachimbaji wadogo wa almasi, ambao nao wamepunguza kasi ya uchimbaji sababu ya kuogopa kupata maambukizi ya corona,"anaongeza Senema. Anasema zamani kabla ya janga hilo la corona walikuwa wakinunua madini ya almasi kutoka kwa wachimbaji wadogo karate tano kwa siku, lakini sasa hivi wananunua karate moja.

Hamza Tandiko ni Mwenyekiti wa wachimbaji wadogo wa Madini Mkoa wa Shinyanga (SHIREMA), anaipongeza serikali kwa kuendelea kuchukua hatua ya kukabiliana na corona, na kuagiza chanjo ya UVIKO-19, ambayo itasaidia kupunguza kasi ya maambukizi.

"Nimesikia mgodi huu wa Mwadui baada ya kusitisha uzalishaji wa madini, wanataka tena kuanza shughuli hizo, hivyo naiomba serikali tutakapoanza tena kununua madini ya mgodi huo zile asilimia tano, ituondolee kodi siziso za ulazima wanunuzi pamoja na mgodi kufuatilia mgodi utuuzie madini kwa bei rafiki," anasema Tandiko.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Emmanuel Johnson, anasema kusitisha uzalishaji wa madini ya almasi Mwadui na El-Hilali, kumewaathiri kwenye mapato, na kwamba katika bajeti zao za mapato ya ndani walikuwa wakitenga Sh. bilioni 1.9, lakini kwa sasa wanakomea Sh. milioni 34, sababu ya kukosa kodi ya ushuru wa huduma wa migodi hiyo.

"Kusitisha shughuli za uzalishaji wa madini kwenye migodi hii halmashauri imeathirika pakubwa sababu mapato yetu ya ndani tunaitegemea, mfano katika mwaka wa fedha 2020-2021 tulikusanya milioni 34, lakini tulikuwa tunakusanya hadi bilioni 1.9,"anasema Johnson.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Dk. Philemon Sengati, anasema mkoa huo ni watatu kuchangia pato la taifa kupitia sekta ya madini, na kwamba kusitishwa kwa uzalishaji wa madini kumewaathiri mkoa pamoja na taifa.

Aidha, Takwimu za uchangiaji mapato mkoani humo kupitia mgodi wa Mwadui zilizotolewa mwaka jana na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Zainab Telack, zinaonyesha kuwa kwa miaka mitatu mfululizo, mgodi huo ulizalisha almasi yenye uzito wa karati 1,175,444.58 zenye thamani ya dola 292,452,648.18.

Kutokana na uzalishaji huo wa madini yenye thamani ya dola 292,452,648, serikali ilipata mrabaha wa Sh. 41,333,031,613.

Mgodi wa El Hilal, kwa kipindi kama hicho ulizalisha almasi yenye uzito wa karate 20,282.22, yenye thamani ya dola 4,241,930.79 na serikali ilipata mrabaha wa Sh. 521,151,775,55, hivyo kutokana na migodi hiyo kusitisha shughuli za uzalishaji serikali imekosa mapato.

Naibu Waziri wa Madini Profesa Shukuru Manya, akiwa mkoani Shinyanga kwenye ufunguzi wa maonyesho ya biashara na teknolojia ya madini, anasema corona imeathiri sana sekta ya madini, na hata kufikia hatua baadhi ya migodi kufungwa na kusitisha uzalishaji.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, na Ajira, Patrobasi Katambi, anasema kufungwa kwa migodi sababu ya changamoto COVID 19, ni hasara kwa taifa kwa sababu ya kupoteza mapato, pamoja na ajira kwa vijana.

"Mtanzania yeyote anapopoteza ajira, kama taifa tunaathirika, sababu mtu huyu lazima aanze kutafutiwa, au kutafuta kazi mbadala ya kumuingizia kipato halali na kuendesha maisha yake...," anaongeza Katambi.

Anasema, serikali inatoa pole kwa migodi iliyositisha uzalishaji wa madini, na kuwakaribisha kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kuzungumza na Wizara za Uwekezaji na ile ya Madini, ili wapate ushauri na kusimama tena kwenye biashara zao na kukuza uchumi wa taifa.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Idara ya Umoja wa Mataifa ya Uchumi na Masuala ya Kijamii (DESA) ya Aprili mwaka jana, uchumi wa dunia unaweza kushuka kwa asilimia 0.9 kutokana na corona, kwa vile ya shughuli nyingi za uchumi zinasimama na nyingine kupunguza kasi ya uzalishaji mali.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Dk. Yudas Ndungile, bila kutaja takwimu za wagonjwa na vifo anathibitisha kuwapo kwa ugonjwa huo, mkoani humo na kuwataka watu wachanje.

Anasema ugonjwa upo na wananchi wanakufa akiwataka kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizo, kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, kuvaa barakoa na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

MAZINGIRA



Watoto wakimbizi wakifuata maji kwenye kambi ya Aden, ambayo hutolewa mara mbili kwa siku. **PICHA: UNICEF**

# Ni kilio, watoto bilioni 1 hatarini athari mabadiliko ya tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

MARA nyingi watu wanapozungumzia mabadiliko ya tabianchi na athari zake, wanawasahau watoto.

Ukweli ni kwamba watoto ni waathirika wakubwa wa tatizo hilo na ni muhimu kuchukua hadhari za kuwalinda ni kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF).

Linaeleza kuwa watoto bilioni moja duniani wako katika hatari kutokana na mabadiliko ya tabianchi, tatizo likiwa kubwa barani Afrika Kusini mwa Sahara.

UNICEF inasema watoto hao ni kutoka mataifa maskini kama Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Nigeria, Guinea na Guinea-Bissau.

Shirika hilo linaeleza kwamba mtoto mmoja kati ya watatu duniani wanaishi katika maeneo ambayo majanga ya mabadiliko ya tabianchi na mazingira yapo, au yanatokea ama yote yanatokea kwa wakati mmoja.

Majanga hayo ni kama ongezeko la joto kali, au baridi, ongezeko la kina cha bahari, mafuriko, vimbunga vya baharini na tufani pamoja na moto wa asili.

Aidha, ripoti ya UNICEF inasema mtoto mmoja kati ya saba duniani kote anaishi katika maeneo yaliyoathiriwa na majanga makubwa matano ya mabadiliko ya tabianchi.

Ripoti inasema vijana na watoto wanaoishi nchini Jamuhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Nigeria, Guinea na Guinea-Bissau ndiyo walio katika hatari zaidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi, yakitishia afya zao.

Pamoja na kukosa afya bora na kutishiwa maisha wanakosa elimu, ulinzi, na kuwaweka kwenye hatari ya magonjwa zaidi , kwa mujibu wa ripoti mpya iliyotolewa UNICEF mwezi uliopita.

"Mgogoro wa mabadiliko ya tabianchi ni mgogoro wa haki za mtoto: Kutambulisha hatari za mabadiliko ya tabianchi kwa watoto ni uchambuzi wa kwanza wa kina unaobainisha hatari ya mabadiliko hayo kwa mtazamo wa watoto wetu."

Ripoti inaziweka nchi katika kiwango chake cha hatari ya athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga mengine ya kimazingira kwa watoto kama vile vimbunga na ongezeko la joto na vile vile kuathiriwa kwao na majanga hayo, kwa misingi ya kutofikiwa na huduma muhimu za kijamii.

"Na watoto hawa wanakabiliwa na kukumbwa na hatari mchanganyiko wa mabadiliko ya tabianchi na majanga mengine ya kimazingira na hivyo kuwawekwa katika hatari kubwa kwa sababu ya kutokuwa na huduma muhimu na za kutosha, kama majisafi na usafi wa mazingira, afya na elimu." Inasema.

Matokeo ya ripoti hiyo yanaonyesha idadi ya watoto walioathiriwa wakati huu lakini takwimu zinaweza kuwa za kutisha zaidi wakati athari za mabadiliko ya tabianchi zikiendelea.

"Kwa mara ya kwanza, tuna picha kamili ya wapi na jinsi watoto wanavyoweza kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi, na picha hiyo ni mbaya sana. Mgogoro wa mabadiliko ya tabianchi na mazingira unadhoofisha wigo kamili wa haki za watoto, kuanzia upatikanaji wa hewa safi, chakula na maji salama, kupatiwa elimu, makazi, uhuru na hata haki yao ya kuishi. Karibu maisha ya kila mtoto yataguswa," anasema Henrietta Fore, Mkurugenzi Mtendaji wa UNICEF.

> "Na watoto hawa wanakabiliwa na kukumbwa na hatari mchanganyiko wa mabadiliko ya tabianchi na majanga mengine ya kimazingira na hivyo kuwaweka katika hatari kubwa kwa sababu ya kutokuwa na huduma muhimu na za kutosha, kama majisafi na usafi wa mazingira, afya na elimu." Inasema.

**ATHARI KWA WATOTO**

Watoto wanaathirika na mabadiliko ya tabianchi kutokana na ongezeko la joto na jua kali. Wanaumia wakiwa nyumbani, wakienda shuleni na wakati mwingine ngozi zao huchubuka na kupata upele unaoambatana na joto hilo.

Kuongezeka kwa joto au baridi kupita kiasi, vumbi linaloambatana na upepo mkali linawaathiri watoto hasa wenye asma, mzio (aleji), magonjwa ya mafuo ambayo kama hakuna huduma za kijamii watoto wanaweza kupoteza maisha.

Matukio ya vimbunga vikali, tufani, mafuriko na moto yanawawaweka kwenye hatari kubwa kwa vile hawawezi kujiokoa, hakuna mikakati ya kuwaokoa tatizo linapotokea.

Aidha, inaelezwa kuwa wanakuwa na hali mbaya kisaikolojia wanapoona nyumba, mali na majengo kama shule wanazosoma yamebomolewa na kimbunga au mafuriko.

Kupoteza wazazi na walezi kwenye mafuriko au majanga kama hayo kunawasababishia kuchanganyikiwa na kuwa na maisha magumu kwa kuwa wanakosa msaada na wanaishi kwa uchungu.

Mabadiliko ya tabianchi yamechangia ongezeko la maradhi kama kuhara kutokana na kukosa majisafi na salama lakini maeneo mengi kukosa huduma za afya majanga yanapotokea.

Aidha, ongezeko la magonjwa kama malaria yanayotokana kuongezeka mbu, yote hayo yanawaweka watoto kwenye hali mbaya zaidi.

Katika sehemu nyingi duniani ukame, upepo, jua kali, mafuriko na ongezeko la viuatilifu kumechangia uhaba wa chakula, njaa, umaskini kutokana na shughuli za kilimo kuathirika na kuvurugwa na majanga ya mabadiliko ya tabia nchi.

Athari zinazotazamiwa ni kwamba kama athari za mabadiliko ya tabianchi hazitadhibitiwa huenda ukuaji wa watoto utakuwa duni kwa sababu dunia itajaa hewa chafu, kutakuwa na eneo dogo la kuishi kutokana na kina cha bahari kuongezeka na kumeza sehemu kubwa za ufukweni lakini ukame na majanga vitachochea uhaba wa chakula.

**UFUMBUZI WA TATIZO**

Shirika hilo linashauri kulinda mazingira ya bahari, kwa kutunza mikoko ili kuzuia vimbunga vya bahari. Linapendekeza pia kulinda misitu na vyanzo vya maji, kupunguza uzalishaji hewa ukaa nyumbani, viwandani na barabarani hasa kunakotokana na injini za magari na vyombo vingine vinavyotumia mafuta na kutoa moshi wenye hewa ukaa, unaochafua mazingira.

Aidha, kujitahidi kubadilisha injini hizo zitumie umeme na gesi ili kuboresha usafi wa hewa yote hayo yafanyika kwa kuelekeza nguvu kwenye kutumia nishati jadidifu (renewable energy) kama umemejua na upepo.

**UN NEWS NA MITANDAO**



# ‘Wasilisheni malalamiko mnapobaini bidhaa bandia’

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka wafanyabiashara na walaji kuwasilisha malalamiko Tume ya Ushindani (FCC), wanapobaini wameuziwa bidhaa bandia.

Naibu Waziri wa Viwanda, Exaud Kigahe, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye majumuisho ya maoni na mapendekezo ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira katika semina iliyolenga kuwaelimisha wajumbe wa kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya FCC.

Alisema wafanyabiashara na walaji wanapaswa kutumia FCC kufikisha malalamiko wanapouziwa bidhaa bandia ili tatizo hilo lishughulikiwe kwa haraka.

Aliagiza FCC kuongeza kasi ya kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa na kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wafanyabiashara na walaji kuhusu hatua za kufuata katika uwasilishaji wa malalamiko wanapoona au kuuziwa bidhaa bandia na jinsi ya kuzitambua.

“FCC wanatakiwa kukagua bidhaa bandia hususani zile zenye madhara kwa maisha ya binadamu kila mara pamoja na kujipanga kukagua bidhaa bandia zinazouzwa kwa njia ya mtandao,” alisema.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, William Erio, alisema katika udhibiti wa bidhaa bandia, kuanzia mwaka 2018 hadi 2021, FCC imefanya ukaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu Dar es Salaam, makasha ya kusafirishia mizigo 1,699 yalikaguliwa huku 545 yakibainika kuwa na baadhi ya bidhaa zilikuwa na nembo za bidhaa halisi na zingine hazionyeshi nchi na mahali zilipotengenezwa.

Erio alisema pia kaguzi za kushtukiza 96 zilifanyika katika maghala na maduka mbalimbali katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Singida, Mbeya, Ruvuma, Arusha na Kilimanjaro.

“Bidhaa zilizokamatwa zilikiuka kifungu cha sita cha MMA ya mwaka 1963 kinachokataza kuuza na kuhifadhi bidhaa zinazonakili nembo halisi,” alisema.

Erio alisema pia walifanya kaguzi za pamoja tisa kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), INTERPOL-TZ na taasisi nyingine za udhibiti za TMDA, Mkemia Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuuna TRA.

Alisema katika ukaguzi huo bidhaa zilizokamatwa ni vifaa vya umeme, ujenzi, vipuri vya magari na virainishi, mafuta na vipodozi. Pia vifaa vya Ofisi, vyandarua, mabegi ya shule, viatu, mavazi, vitaulo vya Watoto, vifaa vya elektroniki, pamoja na vifaa vya nyumbani.

Akitoa tofauti ya majukumu kati ya TBS na FCC, Erio alisema TBS ina jukumu la kusimamia viwango na ubora wa bidhaa wakati FCC inajukumu la kudhibiti bidhaa bandia na kumlinda mlaji.

# Aagiza majengo Mahakama Kuu yakamilike Desemba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, amemtaka mkandarasi wa kampuni ya Arqes African Limited, kukamilisha majengo ya Mahakama Kuu nchini ifikapo Desemba, mwaka huu.

Pia serikali itaendelea kutoa fedha kwa wakati za ujenzi wa majengo ya mahakama ambayo kwa sasa yamegharimu Sh. bilioni 120.

Prof. Ole Gabriel aliyasema hayo wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua majengo hayo iliofanyika jijini hapa.

Alisema hakuna sababu ya mkandarasi kuchelewa kukamilisha ujenzi wa majengo hayo, kwa sababu serikali inatoa fedha kwa wakati na vifaa vipo.

“Ningependa kuona majengo haya yanakamilika kabla ya muda wa mkataba unavyoelekezwa ili yatumike. Ninatamani sana kuona mnamaliza Desemba, mwaka huu halafu vitu vingine vya ukamilishaji vitaendelea ili kukamilisha ujenzi mzima,” alisema.

Alisema serikali inahitaji kuona ujenzi huo unaenda kwa kasi ili kuhakikisha majengo hayo yanakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa jamii kutoka maeneo mbalimbali.

Akizungumzia utoaji fedha, Prof. Ole Gabriel alimshukuru Rais Samia Hassan Suluhu kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

“Wakati naapishwa na Rais moja ya maagizo ambayo nilipewa ni kuhakikisha majengo haya yanakamilika kwa wakati, ikiwamo uwapo wa mazingira mazuri ya wafanyakazi wa mahakama,” alisema.

Alisema mpaka sasa fedha za ujenzi wa majengo hayo zimegharimu Sh. bilioni 120 na kusisitiza serikali itaendelea kutoa kwa wakati ili kuhakikisha zinakamilika.

Aidha, alimtaka mkandarasi huyo ujenzi wa majengo hayo unazingatia uwekaji wa miundombinu ya watu wenye ulemavu.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Godfrey Chibulunje, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu huduma zinazotolewa na mamlaka hiyo hapa nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waganga tiba asili waonywa uvunaji miti ovyo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAGANGA wa tiba asili na watengenezaji wa dawa asili nchini wametakiwa kuacha uvunaji wa miti dawa usioendana na matumizi yake.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akifunga maadhimisho ya wiki ya tiba asili ya Mwafrika kitaifa.

Dk. Gwajima alisema waganga wa tiba asili pamoja na watengenezaji wa dawa asili wanatakiwa kuachana na uvunaji usioendana na mahitaji ili kulinda miti hiyo.

“Hapa kuna shida sana mtu unavuna mti dawa bila kuwa na matumizi nao unakwenda kufanyia nini kupikia kuni, hapa pana shida hebu tuangalie namna ya kuachana na haya ili tunapokwenda kuanzisha mashamba yetu basi tujue kwamba yana ulinzi ambao unaanzia na sisi,” alisema Dk. Gwajima.

Aliwataka waganga wanaokwenda kusajiliwa na waliosajiliwa tayari kuhakikisha kuwa wanafuata sheria zinazoongoza sekta hiyo.

“Sheria nimeona zimebandikwa hapa na nyie mmeziona kanuni na miongozo yote muifute pia mtekeleze miiko na maadili yote mtu akija kijijini akasema yeye ni mganga jamani pale kuna halmashauri ya kijiji ina kamati ya afya huyu mtu atambuliwe.

“Mimi huwa nachoka eti unakuta kitu kimetokea sehemu tena kilikuwa kinajulikana, serikali ya kijiji ipo mtendaji yupo kamati ya afya ipo wenyewe wakiwa na matatizo yao wanakutumia meseji wanakupa waziri, lakini mambo haya wanayakalika kimya sijui wanapewa rushwa,” alihoji Dk. Gwajima.

Kutokana na hali hiyo Waziri huyo aliziagiza serikali za vijiji kwenda kujipanga ili akitokea mganga wa tiba asili katika eneo lao wamuulize kama ana barua na utambulisho wa alikotoka.

Aliwataka waganga wasilalamike kusumbuliwa kwa kuwa wanatakiwa walikotoka kuja na barua ya utambulisho yenye taarifa sahihi na kuripoti kule anakokwenda.

Alisema kwa atakayebainika kufanya hivyo, akikutwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.



# Ileya waridhia kijiji kuingia mpango matumizi bora

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Ileya, Kata ya Ihango Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameridhia kijiji chao kuingia kwenye Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Wamesema wameamua kuridhia mpango huo ili kupandisha thamani ya ardhi yao itakayowawezesha kuinuka kiuchumi na kutokana na ardhi yao kuwa na hadhi ya kutumika kama dhamana wanapotaka kukopa fedha kwenye taasisi za fedha.

Waliridhia mpango huo juzi wakati wataalamu kutoka Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi walipofanya nao mkutano wa kuhamasisha wananchi waukubali mpango huo.

Mmoja wa wananchi hao, Winfrida Mwamkinga, alisema walikubali mpango huo kwa sababu utasaidia kutenganisha shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo makazi, maeneo ya kilimo, maeneo ya malisho na maeneo ya ujenzi wa taasisi za kutolea huduma za kijamii.

Alisema kutokana na kutenganishwa kwa shughuli hizo anaamini mpango huo utasaidia kumaliza migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara kwenye maeneo yao.

"Huu mpango ni mzuri maana kwa mujibu wa maelezo tuliyopewa na wataalamu hawa ni kwamba kutakuwa na maeneo maalumu kwa ajili ya mifugo na mengine kwa ajili ya kilimo, kwahiyo hakutakuwa na mwingiliano unaosababisha migogoro," alisema Winfirida.

Naye Joshua Mwashiwawa, alisema mpango huo ni mzuri na utawasaidia wananchi kuyatumia mashamba yao kujikwamua kiuchumi kutokana na baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa hayatumiki kuanza kutumika.

Alisema yataanza kutumika hata kwa kuyatumia kama dhamana kwenye mikopo kwenye taasisi za fedha kwa madai kuwa mashamba yao kwa sasa yamekuwa na thamani.

Alisema mashamba hayo yatakuwa na nyaraka ambazo zinaonyesha kuwa yanamilikiwa kisheria na hivyo kukubalika kama dhamana kwenye taasisi hizo.

Baada ya wananchi hao kuridhia mpango huo, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Steven Sabala, aliwataka wananchi hao kuzingatia matakwa ya mpango huo ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria.

Alisema mtu yeyote atakayekiuka matakwa ya sheria ndogo zinazosismamia mpango huo na akakiri kosa kwa maandishi, atalipa faini isiyopungua Sh. 50,000.

"Kama mtu atatokea akapanda migomba kwenye eneo la makazi wakati sheria hizi ndogo zinazuia, tutamhoji kwa mujibu wa sheria na akikiri kwa maandishi atalipa Sh. 50,000, hivyo nawaomba wananchi wajitahidi kuzingatia haya masharti," alisema Sabala.

Mtaalamu kutoka Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, John Lulala, alisema upitishaji wa mpango huo ni shirikishi.

Alisema wananchi wa kijiji husika hupewa elimu ili waamue wao wenyewe kuridhia ama kutoridhia na kwamba mpango huo ni mzuri hasa katika kipindi hiki ambacho uchumi unakua.



Wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha Ileya, Kata ya Ihango, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakipitia ramani ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye kijiji chao juzi, kabla ya wananchi kuupitisha mpango huo kwenye mkutano wa hadhara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# H'shauri yakamilisha vyumba madarasa 90%

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imekamilisha mradi mpya wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa asilimia 90 katika Shule ya Sekondari Iduda kwa ajili ya kuanza kidato cha tano na sita katika mwaka wa masomo 2021/2022.

Meya wa jiji hilo, Dormohamed Issa, aliyasema hayo juzi wakati alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo na kusema ujenzi wa shule hiyo ni sehemu ya mikakati ya halmashauri kuboresha sekta ya elimu.

Alisema fedha za ujenzi wa mradi zilitokana na Mfuko wa Jimbo hilo na kwamba msimamizi mkuu wa mradi huo ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa sasa wanaendelea na ukamilishaji wa baadhi ya majengo pamoja na miundombinu mingine.

"Tutahakikisha miundombinu yote muhimu inakamilika kwa wakati yakiwamo mabweni, vyoo na bwalo, miundombinu mingine kama vyumba vya madarasa tayari tumekamilisha vizuri na mbunge wa jimbo letu, Dk. Tulia Akson, ametusaidia pia," alisema Dormohamed.

Fundi mkuu wa mradi huo, Froid Kibona, alisema baada ya kumalizika kwa ujenzi wa madarasa hayo, kinachoendelea kwa sasa ni kuanza kwa ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike.

Alisema wanaanza na mabweni ya wanafunzi wa kike kutokana na kundi hilo kukabiliwa na matatizo mengi tofauti na wa kiume.

Ujenzi wa maabara za kisasa na kuboresha miundombinu ya vyumba vya madarasa ni mkakati mwingine ambao unatajwa na halmashauri hiyo katika kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

# Walalamikia mwenendo wa chuo cha wafanyakazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wafanyakazi wamelalamikia mwenendo usio ridhisha wa chuo pekee cha wafanyakazi nchini kilichopo mkoani hapa wakidai licha ya umuhimu wake wa kupika viongozi wa vyama vya wafanyakazi, lakini hakiendelezwi ipasavyo.

Walitoa malalamiko hayo kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Migodi, Nishati, Ujenzi na kada nyingine (TAMICO) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini uliofanyika katika eneo la chuo hicho kilichopo jijini hapa.

Baadhi ya wafanyakazi walisema chuo hicho kina umuhimu mkubwa wa kuandaa viongozi wa vyama vya wafanyakazi kwa ajili ya kudai na kutetea maslahi yao, na hakipaswi kupuuzwa na kutelekezwa.

Mwenyekiti wa TAMICO Mkoa wa Mbeya, Zege Kokoto, alisema baadhi ya waajiri wanakwepa kuwapeleka wafanyakazi wao kwenye vyuo vya aina hiyo wakihofia kuwa watazijua haki zao na kuzidai.

Alisema fikra za aina hiyo ni za kipuuzi kwa kuwa mara zote wafanyakazi wanaajiriwa ili wamsaidie mwajiri kufanya shughuli zake na kwamba ni muhimu kuwapeleka wafanyakazi kwenye vyuo hivyo.

"Kutelekezwa kwa chuo hiki kunatuathiri sana maana kilikuwa na umuhimu mkubwa sana kwetu sisi wafanyakazi, kinapotelekezwa ni hatari maana hatutakuwa na viongozi wazuri wa vyama vyetu vya wafanyakazi," alisema Kokoto.

Naye Neema Mussa, alisema chuo hicho kinasaidia kuongeza nidhamu ya wafanyakazi kutokana na kufundishwa vitu mbalimbali vya kuzingatia wakati wanapokuwa kazini ikiwamo nidhamu.

Alisema endapo chuo hicho kitatelekezwa taasisi nyingi zitakumbwa na tatizo la nidhamu mbovu ya wafanyakazi hali ambayo itashusha utendaji kazi. Akizungumzia malalamiko ya wafanyakazi hao, Mkuu wa Chuo cha Wafanyakazi cha OTTU, Hezron Kaaya, alisema pamoja na watumishi kuona kama chuo hicho kimetelekezwa, lakini mpaka sasa kimefikia hatua nzuri.

Alisema alipokuwa anaingia chuoni hapo alikuta kuna hoja ambayo inaibuliwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), kwamba chuo hiko kifutwe jambo ambalo sio sahihi.

"Huwezi ukawa kiongozi mzuri wa chama cha wafanyakazi bila kupita kwenye chuo hiki, sasa kazi tuliyonayo sasa hivi ni kukiinua chuo ili kiwe na manufaa zaidi hasa kwenye uzalishaji wa viongozi bora wa vyama vyetu," alisema Kaaya.

Akieleza mikakati ya TAMICO ya kuwaendeleza kielimu viongozi wa chama hicho, Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Mhandisi Fred Kipamila, alisema wanakusudia kuimarisha mafunzo kwa wafanyakazi ili kuhakikisha wanakuwa na viongozi bora.

Alisema wanakusudia kuandaa bajeti ya kutosha mwaka ujao kwa ajili ya kuwapeleka watumishi wao kwenye chuo hicho ili wasaidie hata kuboresha sera za serikali.



# HABARI ZANZIBAR

## Wanaofanya biashara holela tiba asili kukiona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amelitaka Baraza la Tiba Asili Zanzibar kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaofanya biashara holela za tiba hizo bila ya kusajiliwa.

Hemed alisema hayo katika maadhimisho ya 19 ya Siku ya Tiba Asili barani Afrika yaliyofanyika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alifafanua kwamba sio jambo la kuridhisha kutokana na wimbi kubwa la waganga wasiosajiliwa kutoa huduma za tiba asilia katika misikiti, masoko pamoja na maeneo mengine ya wazi jambo ambalo linahatarisha usalama wa afya za wananchi.

Aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kuwa makini na kuachana na tabia ya kununua dawa kiholela, ambazo hazijafanyiwa utafiti na kuthibitishwa na mamlaka husika.

Aliwataka wataalamu hao wa tiba asilia kuitumia vyema fursa waliyonayo katika jamii kwa kuacha kusababisha kufarakana miongoni mwa jamii pamoja na kuepuka vitendo vya udhalilishaji kwa watu wanaofika kwao kupata tiba hizo.

Alisema kuwa kitendo cha kuitumia vibaya fursa waliyonayo ya kutoa huduma ya tiba asili kwa wananchi itasababisha kuharibu taswira nzima ya tasnia ya tiba asilia Tanzania na barani Afrika kwa ujumla.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alilitaka Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Zanzibar kuendelea kushirikiana na wizara anayoiongoza kwa lengo la kukuza tiba hiyo, hasa kuona namna bora ya kuanzisha maabara kwa ajili ya kuchunguza dawa asili ili ziwe na viwango sahihi kwa matumizi ya binadamu.

Alisema tiba asili zina mchango mkubwa katika kuisaidia Wizara ya Afya kwa kuwapatia tiba wananchi wa Zanzibar, hasa kwa kuwapatia wagonjwa huduma ya kwanza wanapopata tatizo la kiafya.

Akitoa salamu za Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), Wawakilishi wa Shirika hilo, Dk. Simon Verndelin, alisema shirika hilo limefurahishwa na uamuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kupambana na UVIKO -19 kwa kuwataka wataalamu wa tiba asilia kujumuika pamoja na wataalamu wengine, kwa lengo la kutoa ushauri wao katika kukabiliana na janga hilo.

Alisema Shirika la Afya Duniani kwa kutambua mchango wa tiba asili, limeendelea kuwaunga mkono wataalamu wa tiba hizo kwa kutoa kila aina ya msaada ikiwamo rasilimali fedha kwa ajili ya kufanikisha kazi za wataalamu hao nchini.

"Tumekuwa tukishirikiana na wataalamu wa Tiba Asili kwa kuwawezesha kuwapatia rasilimali kwa ajili ya kuendesha tafiti mbali mbali," alieleza Dk. Simon.

Akisoma risala, Kaimu Mrajisi wa Baraza la Tiba Asili, Muhamed Mshenga Matano, alisema, Baraza limekuwa likiwafahamisha na kuwaelekeza zaidi waganga wa tiba asilia kujua namna bora zitakazoweza kuboresha huduma zao ili ziwe na viwango sahihi vya matumizi pamoja na kuendana na kasi ya kukua kwa teknolojia.

Matano alisema baraza limekuwa likifanya kazi kubwa ya kuwaunganisha waganga kwa kutumia njia ya kuendesha semina elekezi pamoja na mikutano mbalimbali lengo ikiwa kupata nguvu kazi ya pamoja katika kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema, tangu baraza hilo lianzishwe mwaka 2006 limekuwa likifanya ukaguzi na limefanikiwa kuwakagua waganga 624, maduka 156, pamoja na kliniki mbalimbali.

Alisema pamoja na jitihada hizo walizozichukua, mwitikio mdogo kwa baadhi ya waganga kujitokeza na kusajiliwa.

# Mwinyi: Marufuku wakulima karafuu kulipwa kwa simu

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepiga marufuku ulipaji wa fedha za malipo ya karafuu kwa wakulima wanaouza serikalini kupitia miamala ya simu.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi baada ya kukagua ghala la karafuu katika Bandari ya Wete Pemba na kuzindua meli ya abiria ya Ikram.

Alisema karafuu kuanzia kilo moja hadi 50 zilipwe papopapo ili kuwapunguzia mzigo wakulima wa makato ya miamala ya simu. Dk. Mwinyi aliliagiza Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuhakikisha kiwango cha karafuu kuanzia kilo 50 na kuendelea ziendelee kulipiwa kwa miamala ya simu au ya kibenki ili fedha hizo kuwa na ulinzi.

"Nimepokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa wanalalamika wanapouza karafuu zao katika shirika la biashara la Taifa fedha zao zinalipwa kupitia miamala ya simu au huduma za kibenki natoa agizo kuwa karafuu kwa gunia moja la kilo 50 hadi kilo moja wananchi walipwe fedha zao papo kwa papo," alisema Dk. Mwinyi.

Akizungumzia kuhusu meli ya abiria na mizigo ya Ikram ambayo inafanya safari zake kati ya Unguja na Pemba, Dk. Mwinyi alisema ujio wa meli hiyo utasaidia kuchochea maendeleo ya nchi.

Alisema kuwa meli hiyo pia itasaidia kupunguza tatizo la usafiri wa bahari hasa kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Usafirishaji na Uchukuzi, Hamil Bakari, alisema ujio wa meli hiyo ni faraja kubwa na imeongeza idadi ya meli za abiria na mizigo zilizosajiliwa Zanzibar ambazo ni 42 kati ya hizo 32 za mizigo, nne za abiria na mizigo na sita za abiria pekee.

Akiwasilisha taarifa ya shughuli za maendeleo kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mkuu wa Mkoa huo, Salama Mbarouk Khatib, alisema kwa kipindi cha Julai 2021 mkoa kwa kushirikiana na Shirika la Biashara (ZSTC) imenunua karafuu kilo 77,992.5 zenye thamani ya Sh. 1,010,840,000.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akipata maelezo alipotembelea maonyesho ya tiba za asili wakati wa maadhimisho ya 19 ya Siku ya Tiba Asili barani Afrika, mjini Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kongamano kupinga uvunjaji sheria ya vileo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MWANAHARAKATI wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ali Issa Makame, amesema wameamua kufanya kongamano kwa kushirikiana na viongozi wa madhehebu ya dini kupinga uvunjwaji wa sheria ya vileo unaoendelea kufanywa na Bodi ya Udhibiti Vileo Zanzibar (ZLB).

Makame alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, baada ya madai ya bodi hiyo kuvunja Sheria namba tisa ya Vileo ya Mwaka 2020 tangu kuanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais mstaafu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, Mei 11, 2020.

Alisema kwa mujibu wa kifungu cha 33(1) cha sheria hiyo imeweka masharti vibali kwa kampuni za kuingiza pombe Zanzibar mwisho vitatu, lakini mpaka Febuari mwaka huu Bodi hiyo imetoa vibali kwa kampuni nane kinyume.

Makame alisema kifungu cha 28(k) kimeweka sharti la kutoa leseni za baa umbali wa mita 1000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama nyumba za ibada, shule, hospitali na makazi.

"Wanaharakati tumeona wakati umefika kushirikiana na Viongozi wa madhehebu ya dini kuandaa kongamano la kupinga uvunjwaji wa sheria unaofanywa na Bodi ya vileo bila ya viongozi dhamana kuchukua hatua yoyote tangu kuanza utekelezaji wa sheria mpya ya kudhibiti vileo Zanzibar," alisema Makame.

Aidha, alisema kabla ya kufanyika kwa kongamano hilo wananchi katika kila jimbo watapewa nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu kero zinazotokana na kufanyika biashara ya baa katika makazi ya watu pamoja na viongozi wa wilaya na mkoa katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

Makame alisema maazimio ya kongamano hilo yatapelekwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi baada ya viongozi dhamana wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum kushindwa kuchukua hatua dhidi ya wahusika tangu kuanza kuvunjwa kwa sheria ya vileo.

Alisema kabla ya sheria kupitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliweka rasimu ya mswada wa sheria ulijadiliwa katika vikao mbalimbali na kushirikisha wadau vikao vya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri, lakini Bodi ya vileo imeamua kuweka kando sheria kinyume na misingi ya Utawala bora.

Aidha, alisema wakati umefika kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), kufanya uchunguzi dhidi ya bodi hiyo kutokana na mambo yanayoendelea kujitokeza katika biashara ya vileo.

Alisema wakati umefika kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi (BLW) kujitokeza hadharani kupinga uvunjwaji wa sheria unaofanywa na Bodi ya Vileo kwa sababu wao ndio waliotunga sheria kwa madhumuni ya kudhibiti biashara ya vileo baada ya kuwapo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wa Zanzibar.

Upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya udhibiti wa Vileo Zanzibar (ZLB), Abdulrazaki Abdulkadiri, alisema walilazimika kutumia busara na hekima kuweka kando sheria ili kulinda mapato ya serikali na kulazimika kutoa vibali kwa kampuni zaidi ya tatu za kuingiza pombe Zanzibar.

Hata hivyo alisema kama kuna mtu au taasisi inaona kuna sheria imevunjwa ruhusa kwenda mahakamani kwa sababu mahakama ndio yenye jukumu la kutafasiri sheria.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## PATA MKOPO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI

**TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**NEEMA PETRO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0227/0109** kilichotolewa nan baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **MASWA GIRLS mwaka 2007**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa CONTROL NAMBA 9910830118110**

116434502

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SUMMONS BEFORE THE COMMISSION FOR MEDIATION AND ARBITRATION**
**(HATUA YA WITO MBELE YA TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI)**

**(made under regulation 34(1) imetengenezwa chini ya yakanuni ya 34(1)**

**Labour dispute no.(mgogoro wa kikazi na.)**
**CMA/DSM/KIN/270/2021**
**Between/dhidi ya**
**ERNEST SINDENI NGOGO ………applicant(mlalamikaji / mwombaji)**
**Na /and**
**HYDROTANZA TANZANIA LIMITED……….respondent (mlalamikiwa / mjibu maombi)**

**NOTICE TO ATTEND MEDIATION/ ARBITRATIO HEARING**

**(TAARIFA YA KUITWA KUHUDHURIA KWENYE SHAURI LA USULUHISHI/UAMUZI)**

Take notice that the above mentioned mediaion has been fixed for hearing on 10th day of SEPTEMBER year 2021 at 10:00am hours,at DAR ES SALAAM ZONE AKIBA –BIBI TITI ROAD (unaarifiwa kuwa shauri lililotajwa hapo juu linalokuja kwa hatua yausuluhishi/uamuzi limepnagwa kusikilizwa tarehe …mwezi…mwaka 2021..mahali CMA/DSM

Your required to appear before the commission in person and or accompanied by an advocate/person representative as instructed and produce on that day all relevant documents you intend to rely upon in support of your defence.you are further cautioned to remain in attendance until permitted by the commission

Given under my hand and seal of the commission ,this 1st day of SEPTEMBER year 2021

MEDIATOR/ARBITRATOR
COMMISSION FOR MEDIATION AND ARBITRATION

116434402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/184]**
**MAHAKAMA YA MWANZO (W) YA IRINGA**
**WILAYA YA IRINGA MJINI**

**SHAURI LA NDOA 45/2021**

**MDAI: NANCY D/O MFUGALE WA IRINGA**
**MDWAIWA : THOMAS S/O NGUSA WA MWANZA**

KWAKUWA MDAI AMELETA MADAI YAKE YAKUACHANA NA MDAIWA KWAHIYO UNAHITAJIKA KUHUDHURIA BINAFSI TAREHE 14/09/2021 SAA 2:30 ASUBUHI KWA SHAURI HILO,NI LAZIMA KULETA MASHAHIDI WENU NA HATI ZINAZOHUSU SHAURI HILO.

USIPOFIKA SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA.

**HATI HII IMETOLEWA LEO 31.08.2021**
HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI.

116434802

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.260/2021**

Ombi la **PASTORY SALVATORY THOMAS** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **AGRIPINA KIMAZE WOKUSIMA** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 06/10/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 01/09/2021**

116434902

**WIZARA YA ARDHI,NYUMBA NA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA.**
**MAHALI MASWA.**
**MAOMBI MADOGO NA.168 YA MWAKA 2021**
**KATI YA**
**SOLILE MACHIYA…………..MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1.NGETE MADIRISHA**
**2.MARY MASHISHANGA**
**3.SHASHINHALE AUCTION MART AND TRADING CO.LTD……..WAJIBU MAOMBI**
**WITO/TAARIFA**

Kwa: **NGETE MADIRISHA POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yenu katika Baraza hili la wilaya ya Maswa.Maelezo ya madai yanaweza kupatika hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi(WSD)kabla ya tarehe 30.09.2021.

Pia unajulishwa kuwa Maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya tarehe 30.09.2021 saa 2;30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya-Maswa.

Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 30.08.2021.

**J.T.KAARE**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA(W)**
**MASWA**

116435302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAJABU YUSUPH KIPONZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LEXUS** **y**enye namba za usajili **T889BZT** Lenye chases namba **SXU100029868** Injini namba. **5SFE 88754** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/427317/2021**

116435402

## ANATAFUTWA

Mimi **Zainabu Coster Mowo** wa Dar Es Salaam **P.O.Box 76918** namtafuta bwana **IBRAHIM KHAMIS MOHAMED** wa Dar Es Salaam **P.O.Box 61438** kwa ajili ya kufanya mabadiliko ya majina ya Hati ya kiwanja **Plot na.245,block G** mbezi beach ,tafadhari naomba au kwa yeyote atakayemuona au kufahamiana nae awasiliane nami kwa namba zangu

**Simu: 0787 440022 au 0715 881988**

116434302

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Njile Ngholo Mbusi** Mkazi wa wilaya ya Itilima Mkoani Simiyu anatangaza kupoteza kadi yake ya pikipiki aina ya **FEKON namba 125** yenye namba za usajili **MC 138BZE,** Injini namba **157FMI218FO2442** na cheses namba **LDAPAJOBXJGBO2442** yoyote atakayekuwa ameiokota aiwasilishe katika kituo cha polisi Bariadi . Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa namba ya malipo **9918819241392.**

116431302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **TITOS SAMWELY LUKUMAY** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya gari aina yake **ISUZU(TRUCK)** yenye usajili Namba **T 698 AYD** Chasis Namba. **NPR61L7103993** Engine Namba.4BG1148631 Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Rb Namba. **MOR/MOR/RB/366895/2021.**

116434702

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **EMELIA HAUSI MWAMBAGI** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya pikipiki aina yake Haoujue yenye usajili namba **MC 223 CWY** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Rb Namba. **MOR/MOR/RB/427719/2021**

116435102

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KIPANDE MIKIDADI HUSSEIN** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TOYO KE 14,150CC** yenye namba za usajili **MC 796 AET** chasis namba **KE14KEF0003350,**engine namba **162FM-JE1258765,**yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KGT/TRA/RB/487/2021**

116435940 2

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 90 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**MAGRETH NJIBA MADUMA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY SOPHIA JEREMIA NJIBA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75of Probate Rules)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 22ND Day of September, 2021.
Dated at Dodoma this 24th day of August 2021

……………………………………
**PETITIONER**
Presented for filling this 1st day of September, 2021

……………………………………
**MAGISTRSTE**

116436302


## NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA





TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikata utepe kufungua rasmi tawi la Benki ya Mwanga Hakika Microfinance (MHB), jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Naibu Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson na (kulia kwake) ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki hiyo, Mhandisi Ridhuan Mringo na Naibu Gavana wa Benki Kuu (BoT), Dk. Benard Kibesse. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Simbachawene ataka Magereza kubadilika

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, aliliagiza Jeshi la Magereza kurekebisha mifumo ya utunzaji wafungwa kwa kuwa mifumo iliyopo bado ni ya kikoloni.

Amesema wafungwa hao bado ni binadamu wanahitaji haki pamoja na kuwa wana makosa.

Simbachawene aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa maofisa Magereza Waandamizi kutoka Tanzania Bara, wenye lengo la kufanya tathmini ya kazi zilizofanywa ndani ya jeshi hilo.

Alisema wafungwa ni nguvu kazi ambayo inatumika katika kazi mbalimbali, hivyo jeshi hilo linapaswa kuwaangalia katika suala zima la mavazi, kuzingatia muda wao wa kupumzika na vitu vingine ambavyo binadamu wengine wanastahili kupata.

"Ninaomba uongozi wa jeshi mliangalie hilo. Nimeamua kulisema hapa kwa sababu nimeona katika suala zima la mavazi, malazi, muda wa kupumzika na vitu vingine," alisema Simachawene.

Alisema ufike wakati mfungwa awe na mavazi mazuri ya Ijumaa na Jumapili hata kama hawaendi kusali, waonekane tofauti na mavazi wanayotumia katika siku zingine za kazi.

Waziri alisema wanahitaji kurekebishwa kwa hiyo lazima watunzwe kimaadili ili nao wajione wanapaswa kuwa sawa na binadamu wengine tofauti yao iwe tu mavazi na adhabu ambazo wanastahili kupata.

Kuhusu miradi inayotekelezwa na Magereza, aliwapongeza na kuwataka kutoa haki na kipaumbele kwa gereza ambalo litafanya vizuri na kupewa motisha ya kutatua changmoto na kiasi cha fedha zinazopatikana ziende makao makuu.

# Makinda aonya siasa katika sensa

**Na Julieth Mkireri** KIBAHA

SPIKA Mstaafu wa Bunge, Anne Makinda, ameonya wananchi kuingiza masuala ya kisiasa kwenye sensa ya watu na makazi, inayotarajia kufanyika mwakani na ile ya majaribio itakayofanyika mwezi huu.

Makinda ambaye ni Kamisaa wa Sensa Tanzania, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wakazi wa Mtaa wa Muheza, Wilaya ya Kibaha, eneo ambalo ni kati ya vituo 13 vitakavyoshiriki sensa ya majaribio inayofanyika usiku wa Septemba 10 kuamkia 11.

Alisema kupitia sensa ambayo inatarajiwa kufanyika mwakani, serikali inaweza kupanga mipango ya maendeleo bila shida, hivyo ni vyema wananchi wakaacha kuingiza mambo ya kisiasa kwenye kazi hiyo.

Kutokana na umuhimu huo, aliwataka wananchi kuwa tayari kutoa taarifa sahihi kwa karani atakayekuwa anaandikisha na kwamba taarifa hizo zitatunzwa kwa manufaa ya serikali katika kutekeleza majukumu yake.

"Ni marufuku kwa karani kutangaza habari za mtu. Mwananchi usiwe na sababu ya kutojiandikisha, semeni ukweli mtakapokuwa mnatoa taarifa zenu ziko sehemu salama," alisisitiza.

Makinda alisema uzinduzi wa sensa utafanywa na Rais Samia Suluhu mwezi huu baada ya kufanyika kwa sensa ya majaribio katika vituo 13 ambavyo tayari vimeainishwa.

Alisema kufanyika kwa sensa kutaisaidia serikali inapotekeleza miradi inayofikisha huduma za kijamii kwa wananchi kuwa na takwimu sahihi ya wanufaika.

Sensa ya 2022, kwa mujibu wa Makinda, itakuwa ya tofauti na zilizotangulia kwa kuwa itaanzia ngazi ya vitongoji tofauti na awali ambayo ilikuwa inafanyika kwenye wilaya.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema kufanyika kwa sensa ni jambo la muhimu kwa mkoa wake ambao una migogoro ya ardhi, kujua namna ya kupanga mifugo na watu kwenye maeneo husika.

Kunenge alisema sensa itasaidia pia mkoa huo kupanga masuala ya kiuchumi, mipango miji na viwanda ambapo alieleza kuwa kwasasa ipo sensa ya mifugo inaendelea kufanywa katika mkoa wa Pwani.

"Sasa hivi mkoa una migogoro ya wakulima na wafugaji bila kujua idadi ya watu na mkfugo ni ngumu kupanga idadi gani ya mifugo inahitajika kwenye eneo husika," alisema Kunenge.

Ofisa wa Sensa, Said Ameir, alisema karani ambaye atabainika kutotunza siri za watu ipo adhabu ambayo inachukuliwa hivyo wananchi wanatakiwa kuwa huru kutoa taarifa sahihi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA ANUAI NA. 107 YA 2021**

**BAINA YA**

**MIC TANZANIA LIMITED** ........................................ **MLETA MAOMBI**

**NA**

**YAKOBO JOHN MASANJA** ...................................... **MJIBU MAOMBI**

**Kwa:**
**MIC TANZANIA LIMITED,**
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Rejea mada hapo juu.

Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii mnamo tarehe **14 Septemba, 2021** saa **3.00** Asubuhi bila kukosa na utetezi wako pamoja na vithibitisho/vielelezo vyako vihusuvyo maombi yaliyofunguliwa dhidi yako na kuviwasilisha Mahakamani tayari kwa kusikilizwa maombi.

Fahamu kuwa kukosekana kwako siku hiyo iliyotajwa, maombi haya yatasikilizwa na kuamuliwa bila wewe kuwepo.

Imesainiwa hapa Dar es Salaam siku ya Jumatatu tarehe **30** Mwezi **Agosti, 2021.**

F. Kiswaga
**KAIMU NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DIVISHENI YA KAZI**

216436602

MECHI KALI
HOME
AWAY
HUNGARY
7.12 | 4.03 | 1.49
ENGLAND

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 468

# SAJILI 5 ZA KUSHTUKIZA DIRISHA LIKIFUNGWA ULAYA



**LIVERPOOL,** England

HILI limekuwa dirisha la uhamisho la kupendeza na la kufurahisha zaidi kwa miaka yote. Kutokana na janga la ugonjwa wa Covid-19, klabu zimekuwa wazi zaidi kuliko hapo awali juu ya kuuza wachezaji.

Tumeona idadi kubwa ya wachezaji wanaobadilishana klabu msimu huu wa majira ya joto. Tulishuhudia mikataba mingi ya gharama kubwa ikienda juu ya mstari na rekodi za uhamisho zikivunjwa. Klabu za Ligi Kuu, haswa, zimekuwa za kushangaza sana juu ya kuimarisha vikosi vyao msimu huu wa majira ya joto.

Tulikuwa na siku ya mwisho ambayo ililingana na nishati ya jumla ya dirisha la uhamisho wa msimu huu wa majira ya joto. Jehanamu yote ilivunjika saa za mwisho za dirisha kufungwa na mikataba mingi ya hali ya juu ikijadiliwa na kukamilishwa.

Bila kuchelewesha zaidi, wacha tuangalie usajili bora wa wachezaji watano uliofanywa siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto.

## #5. LUUK DE JONG KWENDA BARCELONA

Baada ya kuondoka kwa Lionel Messi, Ronald Koeman amekuwa na nia ya kuimarisha safu yake ya ushambuliaji. Huku Sergio Aguero akiwa majeruhi hadi Oktoba. Miamba hao wa Catalunya walikuwa wakianza kukata tamaa juu ya kusajili mshambuliaji mwingine.

Wameweza kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Luuk de Jong kutoka Sevilla. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amejiunga na Barcelona kwa mkataba wa mkopo wa msimu. Pia klabu hiyo ina chaguo la kufanya mpango huo kuwa wa mwisho mwishoni mwa kampeni ya 2021-22.

Barcelona pia walihusishwa na Edinson Cavani na Joao Felix siku ya mwisho. De Jong ni usajili wa dakika za mwisho na hajawahi kuwa katika kiwango kizuri cha kufunga mabao. Alifunga mabao tisa na kutoa asisti moja katika mechi 48 kwenye mashindano yote msimu uliopita.

## #4. DANIEL JAMES KWENDA LEEDS UNITED

Daniel James amekuwa mtumishi mwaminifu kwa Manchester United kwa miaka miwili. Yeye si mchezaji aliyesafishwa zaidi kiufundi na bado ana nafasi nyingi ya kujiboresha. Ikiwa James angeendelea kukaa Man United, hangeweza kupata dakika za kutosha kuhitaji ustadi wake.

James alikuwa karibu kujiunga na Leeds United Januari 2019, lakini mabadiliko ya saa ya mwisho ya mipango kutoka Swansea ilimlazimisha raia huyo wa Wales kubaki. Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hatimaye amejiunga na Leeds United. Ni klabu inayofaa kwa mtindo wake wa uchezaji na bila shaka watafaidika kwa kuwa naye kwenye kikosi chao.

James ni mtu anayefanya kazi kwa bidii ambaye yuko tayari kujiimarika zaidi mwenyewe. Ataionyesha Leeds kuwa pauni milioni 30 zimetumika vizuri.

## #3. SAUL NIGUEZ KWENDA CHELSEA

Saul Niguez alipigiwa upatu kuondoka Atletico Madrid msimu huu wa majira ya joto. Chelsea na Manchester United walikuwa wamehusishwa sana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. Mwishowe, ni 'Blues' ambao wamemwongeza kwenye kikosi chao.

Chelsea ilimsajili Saul katika saa za mwisho za siku ya mwisho ya uhamisho kwa mkataba wa mkopo. Wana chaguo la kumsajili moja kwa moja mwishoni mwa msimu. Saul anajiunga na safu ya kiungo ambayo tayari ina wachezaji kama Jorginho, N'Golo Kante na Mateo Kovacic.

Chelsea sasa wana kikosi ambacho kinaweza kutoa changamoto kwa pande zote na mkurugenzi wa Chelsea, Marina

## HABARI MICHEZO

# ,576,020



Granovskaia alisisitiza vivyo hivyo.

**#2. EDUARDO CAMAVINGA KWENDA REAL MADRID**

Real Madrid wamemsajili kiungo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 18, Eduardo Camavinga kutoka Rennes kwa mkataba unaoripotiwa kuwa na thamani ya euro milioni 30. Camavinga amehusishwa na kuondoka wakati wote wa majira ya joto na Manchester United pia inasemekana walikuwa kwenye mbio za kumsajili.

Lakini kiungo huyo alikuwa na ndoto kubwa ya kutaka kuondoka kwenye klabu hiyo, ila alikuwa hapewi nafasi ya kwenda kule Santiago Bernabeu. Real Madrid baada ya kumkosa Kylian Mbappe wakahamia kwa Camavinga na kumsajili siku ya mwisho.

Kwa hiyo, makubaliano ya Camavinga yalishangaza mashabiki ambao wanafurahi juu ya kusaini moja ya matarajio bora ya safu ya kiungo katika biashara hiyo. Kama kiungo wa kati anayefanya vizuri katika jukumu la kushikilia timu, Camavinga atahitaji kushindana na Toni Kroos, Luka Modric na Fede Valverde kwa kila dakika.

**#1. ANTOINE GRIEZMANN KWENDA ATLETICO MADRID**

Kwa kweli limekuwa dirisha la uhamisho la kusisimua na kuona wakubwa kurudi kwenye klabu zao za zamani. Romelu Lukaku amerudi Chelsea akiwa mfungaji bora. Ujio wa Cristiano Ronaldo kule Manchester United ulisababisha ulimwengu kusumbuka. Kwa hiyo ilikuwa inafaa tu kwamba siku ya mwisho iliona nyota mwingine mashuhuri kurudi kwenye klabu yake ya zamani.

Licha ya uthibitisho kinyume chake, Antoine Griezmann ameondoka Barcelona na kujiunga na Atletico Madrid. Ilikuwa ni hatua ambayo ilishitua. Mshambuliaji huyo wa Ufaransa anajiunga na 'Rojiblancos' hao kwa mkataba wa mkopo wa msimu mzima na kipengele cha kumsajili moja kwa moja kwa euro milioni 40 mwishoni mwa msimu.

Ni mpango ambao unaashiria mabadiliko makubwa ya nguvu huko LaLiga. Mabingwa watetezi Atletico Madrid wana kikosi chenye nguvu mno. Barcelona wamepoteza wafungaji wao wawili bora kutoka msimu wa 2020-21.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot, Mubeen Esmail, kutoka Mtwara akionyesha mfano wa hundi ya shilingi milioni 10. 3 za kitanzania baada ya kuibuka mshindi wa bonasi ya Jackpot kutoka SportPesa. Mubeen alibashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 za Jackpot. Wiki hii Jackpot ya SportPesa imefika shilingi 468,576,020. **PICHA: SPORTPESA**

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/09/21 | 17:00 | Exeter vs Forest Green | 2.95 | 3.24 | 2.31 |
| 02. 04/09/21 | 17:00 | Carlisle vs Salford City | 2.65 | 2.95 | 2.75 |
| 03. 04/09/21 | 17:00 | Oldham vs Barrow | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 04. 04/09/21 | 17:00 | Stevenage vs Swindon Town | 2.54 | 2.94 | 2.89 |
| 05. 04/09/21 | 17:00 | Newport vs Leyton Orient | 2.56 | 2.95 | 2.85 |
| 06. 04/09/21 | 17:00 | Colchester vs Sutton United | 2.38 | 3.03 | 3.03 |
| 07. 04/09/21 | 17:00 | Southend vs Wrexham | 2.54 | 3.22 | 2.63 |
| 08. 05/09/21 | 01:30 | Remo PA vs Botafogo RJ | 2.89 | 3.09 | 2.35 |
| 09. 05/09/21 | 03:00 | Bahia BA vs Fortaleza CE | 2.57 | 3.15 | 2.57 |
| 10. 05/09/21 | 03:00 | Cuiaba MT vs Santos | 2.36 | 3.11 | 2.86 |
| 11. 05/09/21 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Colorado Rapids | 2.49 | 3.46 | 2.70 |
| 12. 05/09/21 | 19:15 | Mirandes vs Las Palmas UD | 2.62 | 2.81 | 2.96 |
| 13. 05/09/21 | 19:30 | Patronato Parana vs Talleres | 2.80 | 2.94 | 2.51 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**ALHAMISI - 02 - SEPTEMBA 2021**

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:10 | 1675 | Japan vs Oman | 1.09 | 7.75 | 22.29 |
| 14:00 | 3482 | South Korea vs Iraq | 1.41 | 3.98 | 7.56 |
| 16:00 | 1412 | Kenya vs Uganda | 2.43 | 2.77 | 3.11 |
| 16:00 | 5905 | DR Congo vs Tanzania | 1.50 | 3.59 | 6.60 |
| 17:00 | 4601 | Belarus U21 vs Iceland U21 | 2.86 | 3.34 | 2.25 |
| 17:30 | 4480 | Armenia U21 vs Faroe Islands U21 | 2.01 | 3.34 | 3.34 |
| 18:00 | 1646 | SK Zapy vs FK Viktoria Zizkov | 3.29 | 3.72 | 1.91 |
| 18:00 | 4009 | Asker vs Floya | 1.14 | 7.16 | 12.58 |
| 18:15 | 4263 | Varde IF vs Horsens | 18.32 | 9.45 | 1.07 |
| 18:30 | 1641 | JJK Jyvaskyla vs PS Kemi | 1.15 | 7.16 | 11.60 |
| 18:30 | 2848 | Hungary U21 vs Israel U21 | 2.27 | 3.29 | 2.85 |
| 19:00 | 1071 | Czech Republic U21 vs Slovenia U21 | 1.64 | 3.71 | 4.63 |
| 19:00 | 1187 | Iran vs Syrian Arab Republic | 1.19 | 5.79 | 12.54 |
| 19:00 | 1219 | CSD Barnechea vs Arturo Fernandez Vial | 2.36 | 2.95 | 3.00 |
| 19:00 | 2270 | Namibia vs Congo | 2.76 | 2.76 | 2.71 |
| 19:00 | 2446 | Georgia vs Kosovo | 2.38 | 3.10 | 3.15 |
| 19:00 | 2594 | Niger vs Burkina Faso | 5.23 | 3.15 | 1.71 |
| 19:00 | 5640 | FC Fredericia vs Viborg FF | 5.03 | 4.35 | 1.50 |
| 19:00 | 5802 | Madagascar vs Benin | 2.15 | 2.91 | 3.49 |
| 19:30 | 1802 | France U21 vs Macedonia U21 | 1.09 | 7.93 | 18.38 |
| 19:45 | 5755 | United Arab Emirates vs Lebanon | 1.25 | 5.03 | 10.63 |
| 20:00 | 2151 | Croatia U21 vs Azerbaijan U21 | 1.08 | 8.73 | 19.40 |
| 20:00 | 3211 | San Marino U21 vs Germany U21 | 48.36 | 24.18 | 1.01 |
| 20:00 | 3573 | Admira Wacker II vs First Vienna | 5.62 | 3.97 | 1.50 |
| 20:15 | 5985 | Skive IK vs Silkeborg | 12.67 | 7.21 | 1.14 |
| 20:30 | 2043 | Maccabi Bney Reine vs Beitar Tel Aviv Ramla | 2.73 | 3.17 | 2.58 |
| 20:30 | 2198 | Hapoel Afula vs Ironi Hasharon | 1.71 | 3.62 | 4.76 |
| 20:30 | 2297 | Varmbols FC vs Motala Aif | 6.39 | 4.84 | 1.37 |
| 20:30 | 2529 | Hapoel Rishon Lezion vs SC Kfar Qasem | 2.00 | 3.41 | 3.61 |
| 20:30 | 2650 | AS Ashdod vs Hapoel Acre | 2.53 | 3.32 | 2.68 |
| 20:30 | 5000 | Bnei Yehuda vs Hapoel Ramat Gan | 2.25 | 3.25 | 3.25 |
| 20:30 | 5050 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Petah Tikva | 1.55 | 3.92 | 5.95 |
| 20:30 | 5275 | Sectzya Nes Ziona vs El Fahem | 1.98 | 3.37 | 3.72 |
| 20:30 | 5798 | Hapoel Raanana vs Ahi Nazareth | 2.27 | 3.23 | 3.13 |
| 21:00 | 1648 | Saudi Arabia vs Vietnam | 1.15 | 6.38 | 14.50 |
| 21:00 | 5307 | Australia vs China | 1.68 | 3.45 | 4.76 |
| 21:45 | 1105 | Lithuania vs Northern Ireland | 4.70 | 3.40 | 1.81 |
| 21:45 | 1233 | Italy vs Bulgaria | 1.11 | 7.87 | 28.67 |
| 21:45 | 1284 | Iceland vs Romania | 2.70 | 3.14 | 2.70 |
| 21:45 | 1443 | North Macedonia vs Armenia | 1.76 | 3.54 | 4.79 |
| 21:45 | 1573 | Sweden vs Spain | 4.60 | 3.60 | 1.77 |
| 21:45 | 1956 | Hungary vs England | 7.12 | 4.03 | 1.49 |
| 21:45 | 3114 | Andorra vs San Marino | 1.44 | 4.00 | 8.61 |
| 21:45 | 3164 | Poland vs Albania | 1.48 | 4.19 | 6.98 |
| 21:45 | 4456 | Czech Republic vs Belarus | 1.22 | 5.82 | 14.05 |
| 21:45 | 5895 | Liechtenstein vs Germany | 34.77 | 13.91 | 1.04 |
| 21:45 | 5973 | Estonia vs Belgium | 35.10 | 11.03 | 1.06 |
| 22:00 | 3070 | Algeria vs Djibouti | 1.01 | 20.38 | 38.82 |
| 22:00 | 4095 | Morocco vs Sudan | 1.12 | 6.59 | 18.42 |
| 23:00 | 2857 | Bolivia vs Colombia | 3.30 | 3.20 | 2.09 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



## RONALDO ATOA NENO UNITED, AMTAJA FERGIE

●●● Ni kama ndoto iliyokuwa kweli, baada ya muda wote nimerudi tena nyumbani, sijawahi...

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo amesema "nimerudi mahali nilipokuwa" pale Manchester United na ametoa shukrani kubwa kwa kocha wa zamani wa klabu hiyo, Sir Alex Ferguson.

United imelipa ada ya awali ya euro milioni 15 kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 kutoka Juventus, muongo mmoja baada ya kuondoka klabuni hapo na kujiunga na Real Madrid.

Amesaini mkataba wa miaka miwili, huku kukiwa na kipengele cha kumwongeza mwaka mmoja.

**"Kila mmoja anayenijua mimi, anajua kwamba sijawahi kuacha kuipenda Manchester United," aliandika kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram.**

"Miaka niliyotumia katika klabu hii ilikuwa ya kufurahisha na kile nilichopitia kilikuwa kinafurahisha.

"Siwezi hata kuanza kuelezea hisia zangu kwa sasa, kwa namna nilivyorudi hapa Old Trafford.

"Ni kama ndoto iliyokuwa kweli, baada ya muda wote nimerudi tena Manchester United, mara zote nimekuwa nikiiamini klabu hii na kwa hakika kurudi kwangu kuna maana kubwa.

"Kwa uhakika asilimia 100 nitakuwa na amani kubwa na kiwango bora cha kuendelea kucheza hapa."

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or aliongeza: "Nimerudi mahali nilipokuwa, ngoja tusubiri kuona kile kitakachotokea."

Ferguson alikuwa kocha wa United wakati Ronaldo alipotua hapo Old Trafford kwa mara ya kwanza, ambako alifunga mabao 118 katika mechi 292 kabla ya kuondoka kwenda Real Madrid mwaka 2009.

## ZISIKUPITE

### REAL WAKWAMA KWA MBAPPE

REAL Madrid haikufanikiwa kwa ofa yao mpya ya euro milioni 220 kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22 katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili. ***(Goal)***

### MARTIAL AIKATAA LYON USIKU

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 25, amekataa nafasi ya kujiunga na Lyon katika dakika ya mwisho ya siku ya mwisho ya usajili. ***(L'Equipe, via Mirror)***

### BEEK ALIKATALIWA

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24, alitaka kuondoka hapo Old Trafford - lakini kocha Ole Gunnar Solskjaer akazuia uhamisho wa mkopo kwa raia huyo wa Uholanzi kwenda Everton. ***(AD)***

### ATLETICO WAIKATALIA MAN U

KLABU ya Atletico Madrid imekataa dau la pauni milioni 18 kwa beki wa kulia wa England, Kieran Trippier, mwenye umri wa miaka 30, kutoka Manchester United, na kuchochea klabu hiyo ya Ligi Kuu England kumzuia mlinzi wake, Diogo Dalot mwenye miaka 22 kuhamia Borussia Dortmund. ***(Sport1, via Star)***

### WAMESHINDWA KWA TRAORE

KLABU ya Tottenham Hotspur haikurudi na mkataba bora kwa winga, Adam Traore baada ya kukataliwa ofa yao ya pauni milioni 30 Jumatatu. Wolves walidai pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic)***

### WOLVES KWA KAMARA

KLABU ya Wolves iliendelea na juhudi zake za kumsaka kiungo wa kati wa Marseille na Ufaransa, Boubacar Kamara mwenye umri wa miaka 21, baada ya jaribio la kumsajili Renato Sanches wa Ureno mwenye umri wa miaka 24, kutoka Lille kukwama. ***(Athletic)***

### WEST HAM YAMKOSA LINGARD

KLABU ya West Ham ilikuwa na hamu ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, kutoka Manchester United, lakini haikuwa tayari kufikia bei ya klabu hiyo ya Old Trafford ya pauni milioni 25. ***(Talksport)***

### NEWCASTLE YASHINDWA

KLABU ya Newcastle imeshindwa na jaribio lao la kumsajili kiungo wa zamani wa England, Hamza Choudhury mwenye umri wa miaka 23, kutoka Leicester baada ya majadiliano kati ya klabu hizo kuvunjika. ***(Sky Sports)***

### FALCAO HUYO VALLECANO

KLABU ya Rayo Vallecano itamsajili straika wa zamani wa Manchester United na Chelsea, Radamel Falcao mwenye umri wa miaka 35 kwa mkataba wa miaka miwili. ***(Marca)***

**HABARI MICHEZO**

## Mayai asifu Samatta kurejea tena Ubelgiji

**Na Tunu Hassan,** TUDARCo

WAKATI mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta, akirejea tena kucheza Ligi ya Ubelgiji baada ya timu ya Royal Antwerp FC ya nchini humo kumnasa kwa mkopo akitokea Fenerbahce ya Uturuki, dakika chache kabla ya dirisha la usajili la majira haya ya joto kufungwa usiku wa kuamkia jana, mchezaji wa zamani wa Yanga na timu ya Taifa 'Taifa Stars', Ally Mayai, ametetea uamuzi wake huo.

Samatta ameweka alama katika soka la Tanzania kwa kufanikiwa kucheza Ligi Kuu England akiichezea Aston Villa akitokea katika klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji ambayo aliisaidia kuwa bingwa kwa misimu miwili.

Lakini sasa amerejea Ubelgiji safari hii akijiunga na Royal Antwerp FC, ambapo baada ya kujiunga na klabu hiyo ya Ubelgiji juzi, Samatta aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram: "Nina furaha sana kujiunga na klabu ya Royal Antwerp FC mpaka mwisho wa msimu, ninachokisubiri kwa hamu ni kuanza kucheza mbele ya mashabiki."

## Simbu, Failuna ndani mbio NMB Marathon

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANARIADHA wakongwe nchini, Felix Simbu na Failuna Matanga, wamejisajili rasmi katika mbio zilizoandaliwa na taasisi ya kifedha ya NMB zijulikanazo kama NMB Marathon zinazotarajiwa kufanyika Septemba 18, mwaka huu.

Katika usajili huo uliofanyika jijini Arusha katika Tawi la NMB Clock Tower, Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper, alisema mbio hizo za hisani zina malengo ya kukusanya shilingi bilioni moja kuchangia tiba kwa ajili ya kinamama wenye matatizo ya fistula, kwa ushirikiano na Hospitali ya CCBRT, ambao wamekuwa na changamoto ya kukabiliana na magonjwa hayo na kushindwa kupata fedha kwa ajili ya matibabu.

Kwa upande wao wanariadha hao, Failuna na Simbu, walisema wanaimani kubwa kinamama watasaidiwa kupunguza changamoto na idadi kubwa ya wanawake wanaoishi na fistula.

"Sisi tunajifua kwa ajili ya kushiriki mbio hizo zenye lengo zuri la kuongeza afya ya washiriki na pia kutibu wenye matatizo ya fistula," alisema Felix Simbu.

# SIMBA QUEENS KUIVAA FAD KAMA FAINALI TIKETI CAF

**Na Somoe Ng'itu,** NAIROBI

ILI kujihakikishia tiketi ya kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutoka Ukanda wa CECAFA, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ally, amesema hawataidharau FAD kutoka Djibouti kwenye mchezo wao wa mwisho wa Kundi A utakaochezwa kesho, Ijumaa kwenye Uwanja wa Moi Kasarani jijini hapa.

**Lady Doves FC ya Uganda ndio vinara wa Kundi A wakifuatiwa na Simba Queens kila timu ikiwa na pointi nne, PVP FC yenye pointi tatu ikifuata na kisha FAD ambayo haina pointi hata moja ikiburuza mkia kwenye kundi hilo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Hababuu Ali, alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kwa sababu wachezaji wa FAD wanacheza kwa kuhamasishana timu nzima na hiyo inasaidia kuongeza umakini.

Hababuu alisema pia wanaimarika kadri mechi zinavyoendelea na anaamini watawapa ushindani katika mechi hiyo itakayoamua hatima ya timu yake kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza.

"Tunatarajia itakuwa mechi ngumu, FAD wanacheza kwa kuhamasishana timu nzima wanaongea uwanjani, ni jambo nzuri kiufundi, inasaidia kwenda na kasi ya mpinzani, tumeliona hilo, tutajipanga na hatutawadharau," Hababuu alisema.

Aliongeza mchezo dhidi ya Lady Doves ulikuwa mgumu kwa pande zote mbili ingawa timu yake ilipoteza nafasi mbalimbali ilizotengeneza katika mchezo huo uliomalizika kwa sare ya bila kufungana.

"Tuna nafasi ya asilimia 90 kusonga mbele katika mashindano haya, hakuna mechi rahisi kwa sababu tunakutana mabingwa wa ligi mbalimbali, wote tumekuja kupambana kusaka tiketi ya kwenda katika fainali Misri," alisema kocha huyo.

Naye golikipa wa timu hiyo, Zubeda Mgunda, alisema wataendelea kupambana kuhakikisha Simba Queens inatimiza malengo yake ya kukata tiketi ya kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunataka kucheza fainali za Afrika, tutajituma na kucheza kwa kiwango cha juu, tunataka kuweka rekodi lakini kuipa Tanzania heshima, tunajua mama Samia anatufuatilia, hatutaki kumwangusha," Zubeda alisema.

Kila Kundi linatoa timu mbili zitakazocheza hatua ya nusu fainali na bingwa wa michuano hii atakayepatikana Septemba 9, mwaka huu, ataiwakilisha CECAFA katika fainali za Afrika zitakazochezwa Novemba mwaka huu nchini Misri.

Tayari FAD imeshayaandaa mashindano hayo na mchezo wake dhidi ya Simba Queens utakuwa ni wa kukamilisha ratiba tu.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper (kulia), akiwaelekeza wanariadha maarufu nchini, Felix Simbu na Failuna Matanga namna ya kujisajili kwa njia ya mtandao kwa ajili ya kushiriki mbio za NMB Marathon 2021, zitakazofanyika jijini Dar es Salaam Septemba 18, mwaka huu. Kushoto ni Meneja wa Tawi la NMB Clock Tower jijini Arusha, Emmanuel Kishosha, walipojisajili wanariadha hao. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *DStv sasa yaja na 'Zigo Kama Lote'*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya MultiChoice Tanzania (DStv), imetangaza kuzindua rasmi kifurushi kipya cha bei nafuu kilichoanza kutumika kuanzia jana, Septemba Mosi, mwaka huu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa kifurushi hicho kinachojulikana kama 'DStv Poa', Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, alisema kinapatikana kwa gharama ya shilingi 9,900 kwa mwezi na kwamba kinaongeza wigo mpana kwa Watanzania kuchagua kifurushi wanachokitaka kulingana na uwezo wao.

"Kuanzishwa kwa kifurushi hiki kunaendana na kipaumbele chetu cha kuwajali wateja kwa kuwapatia huduma bora kwa gharama nafuu kadiri iwezekanavyo. Tunatambua kuwa wateja wetu na wananchi kwa ujumla wanapitia wakati mgumu kiuchumi, hivyo tumetathmini njia bora za kuhakikisha kuwa Watanzania wanaendelea kupata burudani, habari na elimu kwa gharama nafuu zaidi," amebainisha Jacqueline.

Alisema mbali na kifurushi cha DStv Poa kuwa cha gharama nafuu, pia kimesheheni chaneli motomoto zaidi ya 40 za habari, filamu, michezo na burudani kedekede kuendana na matakwa ya wateja wao.

Sambamba na kifurushi hicho, pia DStv imeanzisha chaneli mpya ya 'Maisha Magic Poa' itakayokuwa na vipindi kabambe kama vile 'Ni Yeye' kinachoongozwa na wasanii maarufu TID na Chid Benz, Vichekesho vya Watu Baki, Kipindi maarufu cha vichekesho cha Origino Comedy bila kushahau tamthilia za Kapuni, Sarafu, Mwantumu na Sinema bora za Mambo Moto.

Akitoa maelezo kuhusu kifurushi hicho kipya, Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, alisema kutokana na wingi wa chaneli zilizopo kwenye kifurushi hicho na maudhui yake, wateja wa DStv watarajie 'zigo' la burudani. "Hili ni zigo kwelikweli kwani kuna chaneli zaidi ya 40, na zote hizi kwa bei ya Shilingi 9,900 tu kwa mwezi".

Alisema habari njema zaidi ni kwa wateja wa DStv ambao akaunti zao zina salio linalotosha kuwashiwa kifurushi hicho, kwani ikiwa wataridhia, wataunganishwa na kifurushi hicho cha DStv Poa kwa shilingi 9,900 tu na kuendelea kufurahia burudani kutoka DStv na kwa mteja mpya ataweza kujiunga na DStv kwa shilingi 59,000 tu.

# Michezo

Alhamisi Septemba 2, 2021

Nipashe




Sajili 5 za kushtukiza dirisha likifungwa UKURASA 20

HATIMAYE...




Aliyekuwa Ofisa Mhamasishaji na Msemaji wa Klabu ya Yanga, Antonio Nugaz, katika moja ya mikutano yake na vyombo vya habari kabla ya klabu hiyo kutangaza kuachana naye jana. **PICHA: MAKTABA YETU**

## Simba yaja na 'Noma', jezi

**Na Saada Akida**

JOTO la Tamasha la Simba Day limeanza rasmi baada ya klabu hiyo kufanya rasmi uzinduzi wa kuelekea tamasha hilo huku ukitangaza rasmi tarehe ya uzinduzi wa jezi zake za msimu mpya wa 2021/2022 pamoja na kibao kitakachobamba siku hiyo cha 'Simba ni Noma'.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ezikiel Kamwaga alisema awali ilikuwa ni Agosti na sasa wamebadilisha, kuanzia Septemba Mosi hadi 25 ya kila mwaka itakuwa mwezi wa Simba.

Alisema msimu huu wanaanza kwa kuzindua jezi kupitia mzabuni mpya ambaye ni Mtanzania, Fred Ngajiro maarufu 'Fred Vunjabei' kupitia 'Vunjabei Group' baada ya kushinda tenda ya biashara ya kuuza na kusambaza bidhaa za klabu hiyo.

Kwa upande wa Vunjabei, alisema uzinduzi utakuwa na matukio ya aina mbili, wa jezi na vifaa vya michezo ambao utafanyika Septemba 4, mwaka huu, ukionyeshwa katika mitandao pamoja na mubashara kupitia Azam TV.

Alisema wanaenda kuwapa heshima vijana na kutowaangusha mashabiki wa Simba kwa kuhakikisha wanatoa vifaa bora na halisia ikiwa jezi za wachezaji pamoja na mashabiki ambao wanaweza kuvaa hata wakiwa ofisini siku ya mwanzo wa wiki.

"Niweke wazi kwamba hadi sasa hakuna mtu yeyote ambaye ameona jezi mpya au kuenea katika mitandao ya kijamii, jezi itaonekana rasmi Septemba 4, mwaka huu, 'dizaini' ya Simba kwa sasa tuko tofauti na klabu nyingine hapa nchini," alisema.

Mbali na tukio hilo pia msanii wa muziki wa kizazi kipya, Mtanzania, Whuzo, amesema ameshirikiana na msanii kutoka DR Congo, Donat Mwaza, kutunga nyimbo maalum wa Siku ya Tamasha la (Simba Day) itakayokwenda kwa jina la 'SIMBA NI NOMA', Septemba 19, mwaka huu.

# YANGA SC YATANGAZA KIKOSI KAZI, NUGAZ 'OUT'

### Gumbo, Bin Kleb, Davis Mosha wapewa jukumu zito, wakati Djuma naye akirejea mazoezini baada...

**Na Tunu Hassan,** TUDARCo

KLABU ya Yanga imejipanga upya baada ya kuunda 'kikosi kazi' chake cha mashindano kutokana na kilichokuwapo awali kumaliza muda wake wa miaka miwili kwa mujibu wa katiba yao, lakini ikitangaza kuachana na Ofisa Mhamasishaji, Juma Khatib Nugaz, maarufu kama Antonio Nugaz.

**Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo jana, ilieleza: "Uongozi un atoa shukrani za dhati kwa ali yekuwa mfanyakazi wake Juma Khatib Nugaz, maarufu kama Antonio Nugaz kwa utumishi wake ndani ya klabu ya Yanga katika kipindi cha miaka miwili.**

"Ndugu Juma (Nugaz), amemaliza mkataba wake wa utumishi katika klabu ya Yanga, hivyo uongozi umeamua kutoongeza mkataba huo na kwamba unamshukuru sana kwa kazi yake na kumtakia kila la kheri na mafanikio katika maisha na kazi zake nje ya klabu ya Yanga."

Akizungumzia alivyopokea taarifa hiyo, Nugaz alisema: "Kwa udhati wa moyo wangu naomba niwashukuru kuanzia uongozi wote wa Yanga chini ya Mwenyekiti wetu, Dk. Mshindo Mbette Msolla na Kaimu Katibu Mkuu Mpya, Senzo Mbatha Mazingiza, wafanyakazi wenzangu wote kwa upendo wenu kwa kipindi chote cha miaka miwili niliyoitumikia Yanga kwa moyo Mkunjufu na kujitoa kwangu. Mungu awabariki, awalinde na awape kila hitajio la nafsi zenu ili tuweze kuipeleka mbele Brand ya Yanga.

"Wanachama, wapenzi na mashabiki wa Yanga ninyi mmekuwa na mimi kwa moyo mmoja, ahsanteni sana, nawapenda sana na nitaendelea kuwa nanyi. Tutaonana tena hivi Karibuni. Insha Allah."

Katika hatua nyingine, kuelekea msimu mpya wa 2021/22, Kamati ya Utendaji ya Klabu ya Yanga chini ya Mwenyekiti, Dk. Mshindo Msolla, imeunda Kamati mpya ya Mashindano yenye wajumbe wanane (8).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, Kamati hiyo ya Utendaji imemteua Rodgers Gumbo kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano huku wajumbe wakitajwa kuwa ni Hamad Islam, Lucas Mashauri, Abdallah Bin Kleb, Davis Mosha, Seif Magari , Eng. Hersi Said, Pelegrinius Rutayunga na Arafat Haji.

Ikumbukwe hivi karibuni Dk. Msolla alitangaza kuwa kamati iliyokuwapo awali ilimaliza muda wake, hivyo Kamati ya Utendaji imeteua 'kikosi kazi hicho kipya' kushika majukumu hayo.

Wakati huo huo, kikosi cha Yanga kimeendelea na mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Rivers United ya Nigeria huku beki kiraka Shaban Djuma akiungana na wenzake jana baada ya kukosekana juzi mazoezini.

Kwa mujibu wa ripoti ya kitabibu kutoka klabu hiyo, hakuna majeruhi kwenye kikosi kilichopo kambini Avic Town huku Yassin Mustapha na Mapinduzi Balama wakielezwa kuendelea na programu ya mzoezi mepesi.

Akizungumzia mazoezi ya timu hiyo jana, Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli, alisema: "Mazoezi yalianza jana (juzi) ambapo Djuma na Ntibazonkiza [Said] walikosa kwa sababu mbalimbali, lakini Djuma amerejea na Saido atarejea kesho (leo)," alisema.

Alisema baada ya mapumziko ya siku moja yaliyotolewa na kocha Nasreddine Nabi kwa wale ambao hawana majukumu ya timu za taifa, kikosi kilirejea jana (juzi) na kuanza rasmi mazoezi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >